


UONGOZI

 Asante, Ndugu Williams. Salamu, Ndugu...na mkewe, wajumbe wote hapa kwenye karamu hii usiku huu. Bila shaka ni heshima kuu kuwa hapa. Nimetazamia wakati huu tangu tulipoanza kuja huku.

² Nami—nataka kumshukuru huyo bibi. Siwezi kukumbuka jina lake, Billy ameniambia tu wamenipa kifurushi cha paremende za Krismasi, naye akakileta tu kwenye motokaa muda mfupi uliopita. Huyo dada, siwezi kukumbuka jina lake, ametoka hapa California. Hiyo ilikuwa zawadi yangu ya kwanza ya Krismasi. Kwa hivyo na—nakushukuru kwa ajili yake.

³ Sasa, usiku huu ni...Sasa kule Tucson ni saa tatu na dakika kumi, bali nafikiri ni saa mbili na dakika kumi hapa. Kwa hivyo sisi...Naona kuna kujisikia miongoni watu, mimi huchukua muda mrefu nikihubiri, kwa hivyo na—natumaini... [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. Jinsi...watu wema humu. Nawashukuru.

⁴ Lakini mimi—mimi nimehubiri kupita kiasi, karibu hivyo, usiku huu, nimekuwa nikichukua muda mrefu sana kutoka-kutoka Shreveport na kote nchini (nikija humu) usiku baada ya usiku, na unatikizwa ki—kidogo, mwajua, na baridi, na koo lakauka na kupwewa na sauti. Nilianzia kule Shreveport. Nilipoteza nywele zangu nilipokuwa...miaka michache iliyopita. Nami nilikuwa na kipande kidogo nilichokuwa nikivaa nilipokuwa nikihubiri kule kaskazini, nisipate mafua. Nilienda Shreveport nikakisahau na kweli nikapata mafua. Hizo pepo zikivuna hivyo, bila shaka hujui. Nilipelekwa nje kwa bahati mbaya huku ngozi ikali nyororo, nikiwa na jasho kidogo tu nami ikaniingia kooni hasa; ilinibidi kufunga mikutano mingi. Kwa hivyo nimepwewa na sauti kidogo usiku huu.

⁵ Tunataka kusema tumekuwa na wakati wa ajabu tukija milimani, na mikutano. Usiku uliopita tulikuwa na wakati wa ajabu kule...pamoja na hao ndugu kwenye ule mkutano mwingine. Na kwa hivyo tulikuwa na umati mkubwa sana na hudhurio jema sana, watu wakiwa wanyenyekevu sana na wema. Kwa hivyo inanifanya mimi nijisikie vizuri sana kuwa sehemu ya Wafanyi Biashara wa Injili Yote. Imekuwa... .

⁶ Naona nina Ujumbe, kutoka kwa Mungu. Ni wa kipekee kidogo kwa watu wengine...siwezi kujisaidia kuwa...Sina budi kuwa jinsi nilivyo. Nasi...Sikusudii kuwa tofauti, ni kwamba tu ni—ninaishi katika wakati unaobadilika. Tuna... .

⁷ Mradi tu unajenga ukuta upande mmoja ulionyoka, yote ni sawa, mwa—mwashii anaweza kuendelea moja kwa moja safuni. Bali inapokubidi ugeuze pembeni, hapo ndipo wakati... .

Nasi hatujengi ukuta; tunajenga nyumba, mwaona, kwa hivyo hizi kona hizina budi kuja. Zilikuja katika wakati wa Luther, John Wesley, na wakati wa Kipentekoste; ziko hapa tena. Kwa hivyo sisi . . . ni vigumu kugeuza pembeni. Basi ninashukuru sana kwa . . . Mungu, hata ingawa kumekuwa na shida nyingi, watu wameitikia asilimia miamoja. Kwa hivyo tunashukuru sana, tunamshukuru kila mmoja wenu.

Na sasa kabla hatujafungua Kitabu, na tuzungumze na Mwandishi wake, mkipenda, kwa muda mdogo tu, tunapoinamisha vichwa vyetu:.

⁸ Mungu mpendwa, tuna shukrani Kwako usiku huu kwa heshima ya kumjua Yesu Kristo (Mwokozi wetu) Mwanao na kusamehewa bure kwa dhambi zetu, na kujua ya kwamba Damu Yake imetoshwa ambayo imekwisha kufunika dhambi zetu zote na makosa yetu yote. Zimefutwa kabisa na kutupwa katika bahari ya usahaulifu ya Mungu na Bibi-Arushi Wake atasimama kwenye ile Karamu ya Arushi akiwa msafi, asiyeghoshiwa, apate kuolewa na Mwana wa Mungu. Jinsi tunavyokushukuru kwa utoshelevu huu wote pamoja na imani kujua ya kwamba hatutegemei ustahili wetu, bali katika ustahili Wake pekee, kwa ajili ya yale aliyotutenda. Tunashukuru sana.

⁹ Asante kwa ku—kufanikiwa ambako hawa ndugu walipata kule ng'ambo na nchi hizo kule ambako wao wanaona njaa na kiu cha Mungu. Naomba, Bwana, ya kwamba kama wakirudi tena, ya kwamba hawa watoto waliowaleta kwenye Ufalme watakuwa nyanya za nyanya na babu za babu za watoto watakaowaleta pia. Tujalie, Baba.

¹⁰ Tubariki pamoja, usiku huu, Roho Mtakatifu na atupe sisi mambo tunayohitaji. Funga midomo yetu kwa mambo yasiyotupasa kusema, na ufungue mioyo yetu kupokea yale ungetwambia. Tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu twaomba. Amina.

¹¹ Sasa na tufungue mafungu machache katika Biblia ambayo ningetaka kuzungumza juu yake kwa muda mdogo usiku huu, nayo yanapatikana katika Mt. Marko, sura ya 10.

¹² Nami nilikuwa . . . Miaka michache nilipohubiri, ninge—hata haikunilazimu kuandika muhtasari, ningekumbuka. Na haikunilazimu kuvaa miwani kusoma Biblia. Bali kwa maana nimepita umri wa miaka ishirini na mitano, mara mbili, basi ni vigumu kidogo kwangu ku—kufanya kama nilivyokuwa nikifanya. Na, ni kama motokaa iliyozeeka, bali ningali ninakwenda mbio. Aha—aha, nataka kuendelea kuvumisha hata . . . nitakapoingia takatakani nikaundwe tena. Hiyo ndiyo ahadi.

¹³ Luka Mt. sura ya 10, kuanzia . . . naamini nilisema aya ya 21, iwapo naweza kuipata hapa mahali fulani. Nimekosea, ni Marko Mtakatifu. Samahani.

14 Marko Mt. sura ya 10, na a—aya ya ishirini—. . . kuanzia aya ya 21, nataka kusoma. Hebu tufungue aya ya 17 hasa:

Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio, akimpigia magoti chini, akamuuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?

Yesu akamwambia, Kwa nini kuniita mwema? hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu

Wazijua amri; Usizini, Usiue, Usiimbe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu baba yako na mama yako.

Akamwambia, Mwalimu, haya yote nimeyashika tangu utoto wangu.

Kisha akasema. . . Yesu akamkazia macho, akampenda, akamwambia, Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo ujitweke msalaba wako, unifuata.

Walakini yeye akakunja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

Mungu abariki kusomwa kwa Neno Lake.

15 Sasa, tutazungumza usiku wa leo juu ya somo fulani. Nataka maneno yenyewe yawe “Unifuata,” nalo somo langu: *Uongozi*.

16 Naam, ni jambo ng’eni, lakini nalifikiria labda, leo katika kuomba. . . Nami nimekuwa nikichukua muda mrefu, na kila usiku kote katika Ujumbe nilio nao, ambao Mungu amenipa kuutangaza. Nalifikiri usiku huu, humu katika mkutano huu mpya, ningeliendea katika njia nyingine. Na mara nyingi tumezungumza juu yake, tukauita, “Yule Mtawala Kijana Tajiri.” Na—na wengi wa wahudumu humu, ndugu zangu, bila shaka wameuendea katika njia nyingi mbalimbali. Nami nataka kuuendea ka—katika njia tofauti usiku wa leo kuliko vile nimewahi kuuendea, huu *Uongozi*.

17 Hili, kumbukeni hili, ya kwamba kila mmoja wetu, vijana kwa wazee hatua ya kwanza uliyowahi kupiga, ilikubudi kuongozwa na mtu fulani. Hiyo ni kweli. Na hatua ya mwisho ambayo utapiga, mtu fulani atakuwa akikuongoza. Mtu fulani hana budi kuongoza.

18 Mungu ametulinganisha na kondoo. Na iwapo ye yote anajua juu ya kuwafuga kondoo na tabia ya kondoo, naam, unajua ya kwamba kondoo hawezi kujiongoza. Hana budi kuongozwa. Hata machinjioni, tunaona ya kwamba watu huwaleta kondoo mle naye anaongozwa hata machinjioni na mbuzi. Mbuzi humwongoza pale juu, kisha anapofikia ukingoni mwa lile shimo yeye huruka akaliepa, naye kondoo hundelea moja kwa

moja hata machinjioni. Kwa hivyo wao. . . Tunaona ya kwamba kondoo hawezi kujiongoza.

¹⁹ Nakumbuka kisa changu na mmoja wao, wakati mmoja. Nilikuwa mlinzi wa wanyama katika Indiana, nami nilikuwa kule mbugani; nikasikia kitu, mlio wa kuhuzunisha sana. Na ilikuwa mwa—mwana-kondoo, alikuwa a—amepoteza mamaye. Naye hangeweza kwenda alipokuwa mamaye, na mamaye hangeweza kupata njia ya kumfikia yu—yule mwana-kondoo. Nami nikamchukua maskini mtoto huyo, na jinsi alivyotulia akinilalia. Nami nikaenda kule, huku mikono yangu imemshika maskini mtoto huyo. Na kulia, na—nami nikamsikia, jinsi yeye. . . alilala raha mustarehe huku ameeemesha kichwa chake kwangu na ilionekana kama alijua ya kwamba ni—ni—ningemsaidia.

²⁰ Naliwaza, “Ee Mwamba wenye Imara, Kwako nitajificha, nitwae niweke kwenye mikono ya Bwana Yesu,” nami nitaridhika kwa kuwa najua ni—nitaenda Nyumbani kuwa pamoja na wapendwa wangu.” Nami nikawaza, “Mwishoni mwa safari ya maisha yangu, nilete tu mikononi Mwako, Bwana, hivyo. Hivyo najua nitabebwa nivushwe mtoni wakati huo, kule upande wa pili ambako hakutakuweko huzuni na magonjwa, na kadhalika, nami nitakuwa pamoja na wapendwa niliowapenda.

²¹ Na kama utachunguza maumbile, kuna jambo kuu katika maumbile. Kila kitu ni—nikitazamacho, na ambacho Mungu ameumba, Yeye ndiye Mwazilishi wa maumbile. Maumbile yako katika mfulululizo. Maumbile yote kuwa vivyo hivyo. Waona, kila kitu. . . Kama nilivyosema, naamini jana jioni, ya kwamba “Maumbile humshuhudia Mungu.” Kama hujakuwa na Biblia kamwe, ungalitazama maumbile na kujua ya kwamba Biblia hii ni Kweli.

²² Ni—nilipata majaliwa ya kuzunguka-zunguka ulimwengu. Nami nimesoma mambo mengi, na kuona dini mbalimbali; Waislamu, nami nimesoma Kurani, na—na kuona Washiite, Wajaini, Waislamu, na Wabudha, na kadhalika. Hata hivyo, kila moja yao, zote zina filsofia fulani na ki—ki—ki—kitabu cha kanuni za imani na kitabu cha torati, na kadhalika. Bali Biblia yetu ni Kweli, na Mungu wetu ndiye tu aliye sahihi; maana kila mmoja wao hana budi kuelekeza kidole kwenye kaburi mahali fulani ambamo mwanzilishi wao yungali analala, bali Ukristo huelekeza kindole chake kwenye kaburi wazi na unaweza kuishi katika Uwepo wa Yeye Yule aliyewekwa mle. Yeye yu hai! Si Mungu *aliyekuwako*, ni Mungu ALIYE. Si “*Nilikuwa*” ama “*nitakuwa*,” bali “MIMI NIKO.”

²³ Na maumbile yote yako katika mfulululizo, kama nilivyosema, nikinena kuhusu Nyakati zetu za Kanisa (ambazo tuna vitabu vinavyokuja). Zile. . . Nilifanyaje. . . kuhusu kuandika kwangu

kwa zile Nyakati za Kanisa. Na jinsi tunavyoona Kanisa, jinsi limekomaa, likikua tu jinsi hasa maumbile yote hufanya.

²⁴ Nasi tulikuwa tukinena hivi majuzi jinsi jua huchomoza asubuhi, ni mtoto mchanga, mnyonge sana, hana nguvu nyingi kwake. Na siku inapoendelea, linapata nguvu zaidi, lina nguvu zaidi. Kufikia saa mbili linaingia shule, kama kijana mwanamume au kijana mwanamke. Na yapata saa tano limetoka shuleni, na liko tayari kwa utumishi wa—wake. Ndiposa linapozunguka hata yapata saa tisa linabadilika, kutoka umri wa makamu hata umri wa uzeeni. Kisha linakufa jioni. Je, huo ndio mwisho wa jua? La. Linarudi asubuhi inayofuata, kushuhudia ya kwamba kuna uhai, mauti, kuzikwa, kufufuka. Mwaona? Mwaona?

²⁵ Twaichunguza miti, jinsi inavyojimudu na kufanya. Wakati mmoja kule Kentucky, na—napenda kuwinda kindi, nami nikashuka nikaenda kule katika majira ya kupukutika kwa majani, kuwinda pamoja na rafiki yangu. Na ikawa... kukakauka sana.

²⁶ Na mtu ye yote aliyepata kuwinda kindi wa kijivu, ajua jinsi ilivyo vigumu kuwakaribia huku ma—majani yakichakarisha. Ila, jamani, Houdini ni stadi kwa kuponyoka kwa—kwa wanyama hao, jinsi wanavyoweza kutoroka! Ndiposa kujaribu kufyatua baduki upeo wa macho wa yadi hamsini, inahitaji uwindaji mzuri kupata hesabu ya siku moja.

²⁷ Kwa hivyo, Bw. Wood, rafiki yangu, Shahidi wa Yehova a—aliyeongoka, alikuwa pamoja nami. Nasi... Yeye akasema, “Najua shamba humu ambamo mna mtu aliye na wengi sana...” Tunawaita kule, “hollars.”

²⁸ Ni wangapi wanaojua *hollar* ni nini? Vema, mmetoka upande gani wa Kentucky, hata hivyo? Waona? Na huko ndiko ninakotoka.

²⁹ Kama hapa katika moja ya mikutano si muda mrefu uliopita... Nasema haya kwa Ndugu Williams na wengineo, habari zake. Wao walisema, “Tutasimama sasa na kuimba wimbo wa taifa—wimbo wa taifa.”

³⁰ Nami nikasema, “*Nina shauku ya nyumbani kwangu Kentucky.*” Kwa hivyo hamna aliyeimba nami, kwa hivyo... Huo ndio ulikuwa wimbo pekee wa taifa nilioujua. Hivyo basi tulikuwa—tulikuwa sasa...

³¹ Sawasawa, bwana. [Ndugu Branham amepewa kijikaratasi—Mh]: “Tafadhali mwombe bibi fulani sasa humu ndani ambaye anatokwa damu puani.”

Na tuombe:

³² Mungu mpendwa, na...kuomba, Bwana, Wewe ndiwe M—Mponyaji mkuu nami naomba ya kwamba neema Yako na rehema zitamguza mwanamke huyu mpendwa sasa hivi

na kukomesha hiyo damu. Kama watu wanaoamini ambao wamekusanyika pamoja, huyo mwanamke umekuja hapa kufurahia Neno la Bwana pamoja na ushirika wa watu, nami nakuomba, Bwana, sasa hivi, kumkemea adui na kukomesha huko kutokwa na damu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina. (nasi tunaamini . . . ? . . .)

³³ Tuendelee na hiyo hadithi dogo kusudi tupate kujisikia kabla hatujaenda muhtasari mdogo ambao nimeandika hapa, na Maandiko machache.

³⁴ Sasa yeye alisema, “Vema, huyu mzee, tutaenda kule tukamwone. Yeye ana hollar wengi huko kwake,” akasema, “bali yeye ni kafiri.” Akasema, “Kama . . . Angalitulaani kama tungalienda kule.”

³⁵ Nikasema, “Lakini hatuwapati hapa, tumekuwa tukipiga kambi kwa majuma mawili. Nasi tulikuwa wachafu, huku ndevu zimetujaa usoni, hivyo.

³⁶ Akasema, “Vema, basi—basi twende kule.”

³⁷ Basi tukashuka tukaenda maili chache, yapata maili ishirini. Niliisha kuwa mle nchini hapo awali, kwa siku tatu usiku, kwenye kampi ya Wamethodisti ambako kulikuwa na mambo makuu aliyotenda Bwana, na huduma kuu ya uponyaji miongoni mwa Wamethodisti. Kisha tulienda mbali huko tukipanda vilima na hollars na vilele. Na huna budi kujua Kentucky kupajua, ni mahali pa namna gani ulipaswa kupitia. Na tuliporudi kule tukafikia nyumba fulani, na hapo aliketi mzee, wazee wawili, wameketi chini huku wamevalia kofia zao za kale zimeinamishwa juu ya nyuso zao, na—naye akasema, “Ndiye huyo,” akasema, “yeye ni mgumu sana.” Kasema, “Yeye hulichukia neno “mhubiri”. Naye kasema . . .

³⁸ Kwa hivyo nikasema, “Vema, afadhali niketi kwenye motokaa, ama hatutawinda kamwe.” Nikasema, “Nenda kamuulize kama tunaweza kuwinda.”

³⁹ Kwa hivyo akatoka na kuanza kwenda kule, akawazungumzia. Na kule Kentucky, daima wajua, ni “karibu,” na kadhalika. Kwa hivyo akaenda kule na kusema, “Nilishangaa tu kama tungaliwinda kidogo huku kwako.”

⁴⁰ Huyu mzee akiketi pale, karibu umri wa miaka sabini na mitano, huku tumbaku inatiririka kutoka mdomoni mwake, akasema . . . akatema mate na kusema, “Jina lako nani?”

Yeye akasema, “Jina langu ni Wood.”

Yeye akasema, Je, wewe ni wa jamaa ya mzee Jim aliyeishi . . .”

Akasema, “Naam, mimi ni mwana wa Jim.” Kasema, “Mimi ni Banks, Naam.”

41 Vema,” akasema, “Mzee Jim alikuwa mtu mwaminifu.” Kasema, “Bila shaka, fanya upendavyo.” Akasema—kasema, “Uko peke yako?”

Akasema, “La, mchungaji wangu yuko kule.”

Akasema, “Ati nini?”

Akasema, “Mchungaji wangu yuko motokaani,” kasema, “anawinda pamoja nami.”

42 Akasema, “Wood, usiniambie umekuwa duni sana hata inakubidi kuambatana na mhubiri kila uendako?”

43 Kwa hivyo yeye ni mzee, mkali, kwa hivyo nikafikiri ingelifaa nitoke kwenye motokaa, mwajua. Kwa hivyo nikatoka na kuenda karibu, naye akasema, “Vema, wewe ni mhubiri, enhee?”

44 Nikasema, “Naam, bwana.” Akanitazama juu chini (damu ya kindi, na mchafu) naye akasema. . . Nikasema, “Sionekani sana kama hivyo.”

45 Kasema, “Vema, ninapenda hivyo.” Naye akasema, “Wajua nataka kukuambia jambo fulani.” Akasema, “Ninadhaniwa kuwa kafiri!”

46 Nikasema, “Naam, bwana, nafahamu hilo.” Nikasema, “Sifikiri hilo ni jambo la kujivunia sana, hata hivyo. Sivyo?”

47 Naye akasema, “Vema,” akasema, “Sijui.” Kisha akasema, “Nitakwambia niwafikiriavyo ninyi watu.”

Nikasema, “Sawa sawa.”

48 Akasema, “Mnabwekea mti usio na kitu.” Na ni wangapi wanajua maana yake. Mwaona? Maana yake ni mbwa anayedanganya, mwaona; mnyama kamwe hayumo mle juu, mwaona. Akasema, “Mnabwekea mti usio na kitu.”

Nikasema, “Hayo ni maoni yako.”

49 Naye akasema, “Vema,” akasema, “tazama, unaona lile dohani la kale linalosimama kule?”

“Naam.”

50 “Nilizaliwa hapo, miaka sabini na mitano iliyopita.” Naye akasema, “Nimeishi papa hapa kwenye vilima hivi wakati huo wote miaka hii yote.” Naye akasema, “Nimetazama angani, nimetazama huku na huko, na, bila shaka, katika miaka hii yote sabini na mitano, ningeaona kitu kilichofanana na Mungu. Hudhani hivyo?”

51 Nikasema, “Vema, inategemea unatazama nini. Waona, unachotafuta.”

52 Naye akasema, “Vema,” akasema, “Bi—bila shaka siamini kuna kiumbe kama hicho. Nami naamini ninyi watu huondoka tu kwa ujanja kuwaibia watu fedha zao na kadhalika. Na hivyo ndivyo iendavyo.”

53 Nikasema, “Vema, wewe ni raia wa Marekani, una haki ku-kuwazia utakavyo.”

54 Akasema, “Kuna mtu mmoja, wakati mmoja, niliyesikia habari zake,” akasema, “huyo bila shaka . . . Kama yeye . . . Kama ningepata kuzungumza na mtu huyo,” kasema “ningetaka ku-kumuuliza maswali machache.”

Nikasema, “Naam, bwana.”

55 Akasema, “Alikuwa mhubiri, huenda unamjua.” Kasema, “Alikuwa na mkutano humu Campbellsville, si muda mrefu uliopita, kwenye uwanja wa kanisa kule, kambini.” Naye akasema, “Nasahau jina lake.” Kasema, “Anatoka Indiana.”

Na—nami nikasema, “Enhee? Naam, bwana.”

56 Naye Ndugu Wood akaanza kusema, “Vema, mimi . . . (‘Usiseme hivyo.’) Na kwa hivyo akasema . . .

Nikasema, “Na yeye, je?”

57 Akasema, “Vema,” akasema, “bibi mzee . . .” (mtu fulani) “kule mlimani . . .” Kasema, “Wajua, alikuwa anakufa kwa kansa.” Kasema, “Mimi na mke wangu tungeenda kule asubuhi ku—kubadilisha kitanda chake.” Kasema, “Wao hata hawangalimwinua juu kutosha kumwekelea juu ya bakuli la kujisaidia.” Kasema, “Iliwabidi tu kuondoa shuka.” Kisha akasema, “Alikuwa anakufa. Alikuwa ameenda Louisville, na kasema madaktari waliisha mkatia tamaa na kusema ‘atakufa.’”

58 “Na dada yake akaenda kwenye huo mkutano na kusema, ‘Huyo mhubiri anxuwd akisimama pale jukwaani, akawatazama makutano na kumwita mwanamke huyu kwa jina lake, na kumwambia, ‘Alipoondoka, alichukua lesa na kuiweka kibetini mwa—mwake.’ Na kuliita jina la mwanamke huyu chini huku, maili ishirini humu, na kusema jinsi alivyokuwa akiugua kansa, jina lake lilikuwa nani, na yote aliyopitia; kasema, ‘Chukua lesa hiyo na ukaiwekelee juu ya huyo mwanamke,’ kisha kasema ya kwamba ‘huyo mwanamke ataponywa kansa yake.’”

59 Kisha kasema, “Wakaja humu usiku huo.” Kasema, “Hakika, nalisikia kelele za kutisha sana kule. Nilifikiri Jeshi la Wokovu limevamia hicho kilele cha kilima juu kule. Kasema, “Vema,” nikasema, ‘nakisia maskini yule dada amekufa.’ Kasema, ‘Vema . . . Kesho tutaondoka kwenda kuleta gari la kukokotwa, tupate kumchukua tumfikishe kwenye barabara kuu,’ kasema, ‘wapate kumpeleka kwa mzishi.’ Na kasema kuwa . . . Tukangoja. Hamna haja ya kwenda wakati kama huo usiku,” kasema, “yapata maili moja juu humu kilimani.” Kasema, “Tukaenda kule juu asubuhi iliyofuata, na wajua nini kilitendeka?”

Nikasema, “La, bwana.”

60 Yeye akasema, “Huyo mwanamke alikuwa ameketi pale akila keki ya matofaa, na akinywa kahawa, pamoja na mumewe.”

Nami nikasema, “Unamaanisha hayo?”

Akasema, “Naam, bwana.”

“Jamani!” nikasema, “Sasa, bwana, kweli haumaanishi hivyo?”

⁶¹ Akasema, “Inayonitatiza ni...je, huyo mtu, na hakuwa amekuja nchini kamwe, alijuaje hayo.” Waona?

Nami nikasema, “Jamani, huamini hayo.”

Akasema, “Ni kweli.”

Nikasema, “Unaamini hayo?” Waona?

⁶² Akasema, “Vema, nenda moja kwa moja mle kilimani, naweza kukuthibitishia.” Yeye ananihubiria sasa, mwaona.

⁶³ Kwa hivyo ni—nikasema, “Mm mm.” Nikachukua tofaa, ni—nikasema, “Naweza kula moja ya haya matofaa?” Nami nikalipangusa kwa nguo zangu.

⁶⁴ Akasema, “Vema manyigu manjano wanayala, nakisia unaweza kula moja.” Ndiposa...Na sasa nikasema, “Vema—vema...” Ni—nikaliuma...nikaliuma, ni nikasema, “Hilo ni tofaa nzuri.”

⁶⁵ Akasema, “Lo, ndiyo.” Kasema, “Wajuaje? Nalipanda huo mti pale, lo, miaka arobaini iliyopita, ama kitu kama hicho.”

Nikasema, “Lo, hiyo ni kweli?” “Naam, bwana.”

⁶⁶ Nami nikasema, “Vema, na kila mwaka...” “Nikasema, Naona kwamba hatujapata umande ulioganda bado, ni mwanzoni mwa Agosti.” Kisha nikasema, “Majani yanapukutika toka mitini.”

⁶⁷ “Naam, bwana. Hiyo ni kweli, inaelekea majira ya kupukutika kwa majani. Naamini yatakuwa mapema wakati huu.”

⁶⁸ Nikasema “Naam, bwana.” Kabadilisha tulichokuwa tukinena, waona. Naye akasema...Nikasema “Vema mwajua ni ajabu” nikasema, “jinsi huo utomvu unavyotoka kwenye huo mti.” Nikasema, “Kisha hayo majani yakapukutika, na hata hivyo hamna...ha—haijapata umande uliogandamana kuua jani.”

⁶⁹ Naye akasema, “Vema,” akasema, “hayo yanahusianaje na yale tunayonena?”

⁷⁰ Nami nikasema, “Vema, ni—nilishangaa tu.” (Unajua, Mama kila mara alisema, “Mpe ng’ombe kamba ya kutosha na atajinyonga, mwajua.” Kwa hivyo nikampa tu kamba ndefu sana.)

⁷¹ Kwa hivyo akaendelea mbele, na kusema, “Vema, naam, hayo yana uhusiano gani nayo.”

⁷² Nikasema, “Unajua, Mungu huyaleta hayo matofaa nanyi mnafurahia hayo matofaa pamoja na majani, nanyi mnaketi

ki—kivulini na kadhalika. Na unaenda chini katika majira ya kupukutika kwa majani mwakani na” nikasema, “kisha unarudi tena pamoja na matofaa na majani tena.”

⁷³ Naye akasema, “Lo, hayo ni maumbile tu. Waona, hayo ni maumbile.”

⁷⁴ Nami nikasema, “Vema, bila shaka, hayo ni maumbile.” Nikasema, “Hayo ni maumbile, bali mtu fulani hana budi kuongoza maumbile.” Waona, mimi . . . yeye akasema . . . “Hebu niambie ni nini kinachofanya hivyo?”

⁷⁵ Naye akasema, “Vema, bi—bila shaka ni maumbile.”

⁷⁶ Nikasema, “Ni nani anayeliambia lile tawi dogo sasa, na . . . ?” Nikasema, “Basi, sababu ya kuanguka kwa lile jani, ni kwamba huo utomvu hurudi chini kwenye mizizi. Vipi kama huo utomvu ungalikaa mtini katika majira ya baridi? Ingekuwaje?”

⁷⁷ Kasema, “Ungaliuangamiza huo mti.”

⁷⁸ “Vema,” nikasema, “ni busara gani inayoupeleka huo utomvu hata kwenye mizizi, kusema, “Toka humu sasa, majira ya kupukutika kwa makani mwakani kunakuja, ingia kwenye mizizi ukajifiche? Na ukae mle mizizini kama kaburini; kisha Majira ya kupukutika majani yatakapokuja, majira yafuatayo ya kuchanua yatakapokuja tena, utazaa matofaa zaidi, na kuchanua majani na kadhalika.”

⁷⁹ Yeye alisema, “Hayo ni maumbile tu, yatafanya hivyo.” Kasema, “Hall ya hewa! Kule kubadilika, mwajua, kufa kwa majira ya kupukutika kwa majani.”

⁸⁰ Nikasema “Weka ndoo ya maji kule juu ya mti ulioko kule, uone kama maumbile yatayatelemsha chini ya huo mti na kuyarudisha tena. Waona?” Waona?

“Vema,” akasema, “huenda una kitu.”

Nikasema, “Waza hayo tunapoenda kuwinda.”

Naye akasema, “Vema,” akasema, “windeni mnakotaka.”

⁸¹ Nikasema, “Nitakaporudi, iwapo utaniambia ni akili gani inayopeleka huo utomvu uliomo kwenye huo mti ikauingiza mizizini ukakae humo katika majira yote ya baridi na kurudi majira ya baridi yafuatayo, nitakwambia hiyo ndiyo akili ile ile iliyoniambia kuhusu huyo mwanamke kule.”

Kasema, “Iliyokwambia?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Wewe siwe yule mhubiri!”

Nikasema, “Ungejua jina lake?”

Kasema, “Naam.”

Nikasema, “Branham?”

Akasema, “Ndiye huyo.”

Nikasema, “Hiyo—hiyo ni kweli.” Waona?

⁸² Basi mwajuaje? Nilimwongoza huyo mzee kwa Kristo, papo hapo kwa ushuhuda wake mwenyewe.

⁸³ Na mwaka mmoja baadaye nilikuwa kule nikasimamisha motokaa (ikiwa na leseni ya Indiana) uwanjani mwao. Walikuwa wamekwisha kuhama, alikuwa amekwisha kufa. Na kwa hivyo niliporudi, hapo alisimama mkewe kunipura kweli kweli; nami nalifikiri nilikuwa na ruhusa ya kuwinda. Akatoka mle, akasema, “Huwezi kusoma?”

⁸⁴ Nikasema, “Naam, mama.” Akasema, “Uliona ishara za vibao zilizosema “Hamna Kuwinda!?”

⁸⁵ Nikasema, “Naam, mama, bali” nikasema, “ni-nina ruhusa.”

⁸⁶ “Huna ruhusa!” akasema. Kisha kasema, tuliweka hivyo—hivyo vibao humu miaka mingi iliyopita.”

⁸⁷ Nikasema, “Vema, dada, ni—nilikosea basi, nasikitika.”

⁸⁸ Kisha kasema “Kusikitika bure! Hizo leseni za Indiana kule, na kuja mpaka huku, ninyi ni watu wajasiri sana!”

Nikasema, “Naweza kueleza?” Nikasema . . .

“Ndiyo! Nani aliyekupa idhini?”

⁸⁹ Nikasema, “Sijui tu . . .? Nikasema, “Ilikuwa mzee aliyekuwa ameketi pale ukumbini, nilipokuwa humu mwaka uliopita, nami nilikuwa nikinena habari za Mungu.” Waona?

Naye akatazama, akasema, “Wewe ni Ndugu Branham?”

Nikasema, “Naam, mama.”

⁹⁰ Akasema, “Nisamehe. Sikujua u nani.” Akasema, “Nataka kukwambia ushuhuda wake. Katika masaa yake ya mwisho ya kufa, aliinua mikonu yake na kumshukuru Mungu.” Kasema, “Alikufa katika imani ya Kikristo, naye akatwaliwa kwa Mungu.” Mwaona?

⁹¹ “Wakinyamaza hawa, mawe yatapiga kelele papo hapo.” Mna kitu fulani katika maumbile.

⁹² Watazameni ndege, watazameni wanyama, tazameni kila kitu, na tazameni maumbile.

⁹³ Mtazameni hua mdogo anavyoruka. Yeye ni ndege tofauti namna gani, Mwaona. Ye—yeye hana nyongo kamwe, hawezi kula kama kunguru alavyo. Mwaona? Hana nyongo ndani yake. Si lazima aoge ma—ma—majini, kwa maana ana kitu fulani ndani yake; kinamsafisha toka ndani hata nje, mwaona.

⁹⁴ Na hivyo ndivyo alivyo Mkristo. Hivyo ndivyo Mungu alivyojiwakilisha katika—katika—hua. Mwaona, maana . . . na pia . . . Yesu aliwakilishwa kama Mwana-Kondoo. Kila mara katika maumbile utampata Mungu. Naye Mungu alitulinganisha na kondoo ambao hawana budi kuongozwa. Je, Mlitambua

hapo, nilihubiri ujumbe juu yake hivi majuzi? Kwamba Hua alishuka juu ya Mwana-Kondoo—kumwongoza Mwana-Kondoo, naye akamwongoza machinjioni. Huyu—huyo Hua! Basi, kama Mwana-Kondoo. . . Huyu hua hangalitua juu ya mnyama wa aina nyingine ye yote, kwa sababu wote iliwapasa wawe na tabia ile ile. Mwaona? Kama Hua angalitua juu ya mbwa mwitu, angalikoroma ama kunguruma, Hua angaliruka aende Zake.

⁹⁵ Vema, ndivyo ilivyo leo. Na kwa njia zetu mbovu, Roho Mtakatifu huruka na kwenda Zake. Haina budi iwe ni tabia ile ile. Ndege wa Angani, yule hua; mnyama aliye mpole sana duniani, mwana-kondoo; hao wanaweza kupatana. Na Roho Mtakatifu anapokuja juu yetu na kutufanya viumbe vipya, basi anaweza kutuongoza. Bali tukijaribu kuishi maisha yale yale ya kale, haitafaulu! Haitafaulu kamwe.

⁹⁶ Basi hatua ya kwanza ambayo labda ulichukua maishani mwako, tukinena kuhusu uongozi, ilikuwa labda mikono ya mama mzee. Hiyo mikono huenda imekufa usiku huu, huku nje makaburini mahali fulani, bali hiyo ndiyo mikono iliyokushikilia kupiga hatua yako ya kwanza.

⁹⁷ Kisha baada ya mama kukufundisha namna ya kutembea, ungepiga hatua chache kisha ukaanguka, ukainuka, nawe ulifikiri ulikuwa ukitenda mambo makuu, halafu akakupeleka kwa *mwalimu wa shule*. Ndipo akaanza kukuelekeza kwa elimu; mambo yakupasayo na jinsi ya kuyafanya, na jinsi ikupasavyo kujifunza, na—na mambo kama hayo.

⁹⁸ Kisha baada ya mwalimu wa shule kumaliza nawe, basi ukarudi ulikotoka, *baba* yako akakuchukua. Ndipo baba yako alipokuchukua, akakufundisha labda biashara yako; jinsi ya kuwa mfanyi biashara aliyefanikiwa, jinsi ya kufanya mambo yafaayo. Mama yako alikufundisha jinsi ya kuwa m—mke wa nyumbani, jinsi ya kupika, na mambo kama hayo.

⁹⁹ Kisha walipomaliza nawe, ndipo *mchungaji* wako ama *kasisi* akakuchukua.

¹⁰⁰ Lakini sasa ni nani anayekuongoza? Hilo ndilo swali sasa. Sasa, sote huongozwa na kitu fulani usiku huu. Hatuna budi. Tunaongozwa. Tazama!

¹⁰¹ Sasa hebu tumtazame huyu kijana. . . kile kilichomshawishi. Na tuangalie. . . tungemwita huyu kijana mfanyi biashara, maana alikuwa mfanyi biashara. Yeye alikuwa mtu mashuhuri aliyefanikiwa. Hebu tukawatazame viongozi wake.

¹⁰² Labda, kwanza, mama yake aliisha mfundisha alipokuwa mvulana mdogo mambo aliyopaswa kutenda. Babaye alikuwa amemfanikisha sana, na labda akamwachia u—akamwachia urithi, kwa maana yeye mwenyewe alikuwa mtawala; huenda ikawa babaye aliisha kufa, kwa hivyo alikuwa m—mfanyi biashara. Alikuwa. . . Hebu tumwite, leo, kama mfanyi biashara

Mkristo; ama, alikuwa mfanyi biashara wa kidini, nafikiri hayo yangukuwa matamshi bora.

¹⁰³ Mtu huyu alikuwa wa kidini, hakuwa kafiri kamwe. Naye aliisha fundishwa na mamaye jinsi ya kutenda haki, jinsi ya kuenenda, jinsi ya kuvaa. Aliisha fundishwa na babaye, mfanyi biashara mashuhuri, jinsi ya kuwa mtu aliyefanikiwa; na biashara yake ilifanikiwa sana. Na babaye na mamake walikuwa wamekuzwa kanisani, nao walikuwa wamemwelekeza kwa kasisi. Naye kasisi akamfanya mtu wa kidini sana. Kwa hivyo alikuwa mtu muungwana sana, alikuwa mvulana mzuri mwenye tabia njema.

¹⁰⁴ Kama Yesu Kristo alimtaazama akampenda, kulikuwa na jambo fulani katika mvulana huyu lililokuwa halisi. Hiyo ni kweli. Kwa maana Biblia ilisema hapa, tunaona katika Marko, “Na Yesu akamkazia macho, akampenda.” Ndio, “Yesu akamkazia macho, akampenda.” Kwa hivyo basi hapana budi mna jambo halisi la kupendeza sana kuhusu huyu kijana. Alikuwa . . . alikuwa na tabia njema, na maadili mema. Alikuwa mtu aliyekuzwa vizuri; mwenye busara, mwenye akili, mwerevu, aliyefanikiwa katika biashara, na mtu wa kidini. Alikuwa na tabia nzuri ambazo zilivutia sana, hata zikamvutia Mwokozi Yesu Kristo. Bali alipokabiliwa, huku amefanikiwa na mambo haya yote . . .

¹⁰⁵ Hamna jambo lililoenda kombo; yeye alikuwa ametengenezwa vilivyo, akapimika barabara, mwenye busara, elimu inayofaa, ufanisi wake, alikuwa mwenye akili, mfanyi biashara bora, labda alikuwa mwanachama wa kundi fulani la biashara mahali fulani mle Palestina. Huenda alikuwa mshiriki wa ushirika wa wa wafanyi biashara kama tulivyo usiku huu, bila shaka alikuwa hivyo, kwa maana wafanyi biashara daima huwa na ushirika wao kwa wao, mmoja kwa mwingine.

¹⁰⁶ Maana kama tu “watu wa tabaka moja,” wana mambo ya kuzungumza. Na kama hili . . . Watu wa kidini, hawataki kunena habari za mwenye kilabu cha pombe na . . . wote pamoja, maana hawana mambo sawa. Yatupasa kuwa na mambo yaliyo sawa. Kwa hivyo Wakristo huwa na mambo yaliyo sawa na ya Wakristo; wenye dhambi wana mambo yaliyo sawa na—na wenye dhambi, na—na mashirika, na cho chote walicho nacho, wana mambo yaliyo sawa. Na kijana huyu mvulana labda alikuwa mwanachama wa u—ushirika wa wafanyi biashara.

¹⁰⁷ Yeye alikuwa wa kidini kupindukia, kwa maana Yesu, katika kumswali hapa, alisema, “Nimeshika amri hizi, nikazitii zote tangu utotoni.” Hiyo ni kweli.

¹⁰⁸ Mnaona, yeye alikuwa amekuzwa vilivyo, akafunzwa vilivyo, na kadhalika. Bali alipokabiliwa na—na lile wazo la Uzima wa Milele . . . Sasa nawatakeni muone, mbali na hii tabia yote aliyokuwa nayo, alijua bado hakuwa amepata Uzima wa Milele.

109 Sasa, vyama vyetu vyote, kanisa letu, uwanachama wetu, na mambo tunayoyathamini sana, vyama vyetu vya Kiamerika, na kila kitu, ni sawa, hamna neno dhidi ya hayo. Na shirika letu la Wafanyi Biashara Wakristo hapa, ni jambo kuu, limekuwa mlango uliofunguliwa kwangu mimi. . . katika mawazo yangu ya kutokuwa dhehebu maana “sisi ni Wakristo.”

110 Hamna ye yote (hamna dhehebu moja) linaloweza kutudai sisi, Mkristo halisi, maana wewe ni mali ya Mungu. Madhehebu yameundwa na wanadamu, na Ukristo unatoka Mbinguni. Bali katika mambo hayo yote tuliyo nayo, hata yawe mazuri vipi, hata tuje pamoja vipi, na hata tuwe na mikutano mizuri vipi, na tushirikiane vipi, tungali tunakabiliwa kila mmoja wetu na *Uzima wa Milele*. Na haidhuru tumefanikiwa vipi katika biashara, jinsi tumefanikiwa, na hata tuwe wafuasi wa kanisa mashuhuri vipi, na jinsi tunavyotenda kazi, jinsi tunavyojaribu kutenda mambo vizuri, hata hivyo, iwapo haifanywi kwa njia ipasayo, ni kuabudu Mungu bure.

111 Yesu alitamka hayo vivyo hivyo, ninapokoma hapa kwa dakika chache. Yeye alisema, “Ninyi mnaniabudu bure, mkifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.” Sasa waza! Kuabudu kwa moyo mweupe na kwa uaminifu (ukiwa na moyo mweupe) mbele za Mungu, na bado iwe bure! Ilianza hivyo na Kaini, katika Bustani ya Edeni. Kuabudu kwa moyo mweupe, bali kulikataliwa! Kwa kidini sana, bado kulikataliwa!

112 Kule Shreveport juma lililopita, juma lililotangulia lililopita, kwenye mkutano wa Wafanyi Biashara, kule katika kiamsha kinywa kuliko kuwa kumekusanyika watu mia kadha, nalichukua masaa mawili na nusu kuhubiri juu ya: *Kumtumikia Mungu Pasipo Mapenzi Yake* Sasa, hiyo yaonekana ya kigeni, bali hatuna budi kujielekeza kwenye njia iliyoandaliwa na Mungu ya kutenda hayo. Haidhuru tunafikiri ni njema vipi, haina budi iwe kulingana na Neno la Bwana au ni bure. Kaini aliabudu, bali haikuwa kulingana na na Neno la Bwana. Mafarisayo waliabudu, bali si kulingana na Neno la Bwana. Na katika ujumbe huu kwa Wafanyi Biashara, nikafundisha haya.

113 Daudi, yeye alitaka kumtumikia Bwana, na alikuwa kweli katika yake aliyosema. Alisema, “Ni haki kwa sanduku la agano la Bwana kuwa kule chini? Shime, tukalilete humu.” Katika siku za mfalme, yule mfalme mwingine ambaye yeye alimfuata. Akasema, “Si haki. Wao hawakutaka shauri kwa Bwana kwa lile sanduku la agano, bali sisi lazima tufanye hivyo.” Sasa, hiyo ni kweli, waliyopaswa kufanya. Akasema, “Yatupasa kwenda tukajirudishie lile sanduku la agano, na tunaweza, kutaka shauri kwa Bwana.” Na hiyo ni kweli, na lilikuwa mle katika nchi nyingine. Kasema, “Sharti tulilete humu. Tulilete humu na kuliweka nyumbani mwetu humu, tukamwabudu Bwana.”

114 Basi tazameni yeye alitumia njia isiyofaa kufanya hivyo. Yeye alishauriana na maakida wa hamsini na mamia na maelfu. Wote walitakwa shauri, kila mmoja. Yakionekana kuwa ni mapenzi ya Bwana, ilionekana kama kwamba ilikuwa Ni—Neno la Bwana.

115 Neno la Bwana, wakati mwingine inakupasa kuliweka mahali pake ama si Mapenzi ya Bwana. Waona? Hebu hilo liingie ndani sana nawe utapata ku—kufahamu ninayojaribu kusema.

116 Sitaki kanisa lifuate nyayo zile mlizopata kule Uingereza; nywele ndefu, wanaume waliojipaka rangi, na kupotoka. Hatutaki hayo! Haidhuru jinsi inavyosikika ya kidini, hata Elvis Presley aimbe nyimbo za kidini vipi, yeye yungali ibilisi. Nami si hakimu, bali “Kwa matunda yao mtawajua.” Mwaona? Yeye ni Mpetekoste, bali hiyo si kitu. Mwaona, matunda yako yanashuhudia kile ulicho.

117 Haidhuru hata Roho akija juu yake, angalinena katika lugha, angalipasa sauti, angaliponya wagonjwa, naye Yesu alisema, “Wengi wao watanijia siku hiyo, na kusema, ‘Bwana, je, mimi sikutenda *hili* na *lile*?’ Nami nitasema, ‘Ondokeni Kwangu, enyi mtendao maovu, hata sikuwajua kamwe.’” Mwaona?

118 Hatuna budi kuwa Wakristo halisi na wa kweli, na njia pekee tunayoweza kufanya hayo ni kukabilia na swali hili hapa la Uzima wa Milele.”

119 Mna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na hiyo hutoka kwa Mungu. Naye alichagua tangu awali kila kiumbe ambacho kingeupata. Kama tu ulivyokuwa chembechembe hai katika baba yako, ulikuwa chembechembe hai katika Mungu; mmoja wa sifa Zake hapo mwanzo, la, sivyo, hautakuwa Mle kamwe. Wewe ulitoka kwenye tumbo la uzuzi la mama yako; babako hakukujua wewe, ulikuwa viunoni mwake. Na ulipoingia katika tumbo la uzazi la huyo mama, ndipo ukawa mwanadamu na umefanywa katika sura ya baba yako, sasa waweza kushiriki pamoja naye. Naam, ni jambo lile lile kwa Mungu, iwapo una Uzima wa Milele.

120 Huo uhai uliozaliwa nao ule uhai wa kawaida, uhai wa kimwili, huo ulikuwa kwa babako. Na njia pekee unayopitia kwa Kuzaliwa Mara ya Pili, ndiyo njia pekee, haina budi kuwa imetoka kwa Baba yako wa Mbinguni, sifa Zake. “Wote alionipa Baba Yangu watanijia Mimi.” Waona?

121 Wewe uko humu kwa sababu jina lako liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla hata hapajakuwepo msingi wo wote wa ulimwengu. Hiyo ni kweli hasa. Wewe ni chembechembe hai, chembechembe hai ya kiroho kutoka kwa Baba yako wa Mbinguni, sehemu ya Neno la Mungu. Kama hiyo ni kweli, kama nilivyosema, basi ulikuwa pamoja na Yesu alipokuwa hapa kwa sababu Yeye *alikuwa* Neno: uliteswa pamoja Naye, ukafa pamoja Naye, ukazikwa pamoja Naye, na

kufufuka pamoja Naye, na sasa unaketi katika Ulimwengu wa Roho *katika* Yeye!

¹²² Tazameni, Daudi alifikiri kila kitu kilikuwa shwari, naye akashauriana na watu hawa wote, na kila mmoja wao akaanza kucheza na kupiga kelele na kulia kwa sauti kuu. Walijumuika kidini vilivyo, bali hata hivyo haikuwa mapenzi ya Mungu kushuka kwenda kulirudisha Neno la Mungu katika nyumba ya Mungu. Bali, waona, Mungu daima (katika nyakati zote) hutenda kazi kupitia njia moja. Uamuzi Wake wa kwanza ndio uamuzi pekee, kwa sababu Yeye ni mtimilifu katika uamuzi Wake. Yeye hatendi lo lote bila kwanza kuwafunulia watumishi Wake, manabii. Bila shaka.

¹²³ Ndivyo ilivyo sasa. Wakati wa kanisa tunamoishi, hamna kanisa, hamna Methodist, Baptisti, Pentekoste, ama cho chote kile, kinachoweza kulifanya Kanisa hili kuwa Bibi-Arusi. Haina budi iwe ni jibu la Malaki 4, kwa Mungu kutuma nabii akawafunulie, maana hiyo ndiyo njia pekee. Makanisa yetu yalifanyika dhehebu na kutupilia kitu hicho kwenye mchafuko na msongamano, jinsi imekuwa daima, na Mungu kila mara humtuma nabii.

¹²⁴ Basi nchini humu mlikuwemo Nathani, nabii aliyethibitishwa mbele za Mungu, naye hata hawakumtaka shauri.

¹²⁵ Nao wakashuka wakaenda kule na kusababisha uhai wa mtu asiye na hatia, na kadhalika, nao wakachukua lile sanduku la agano. Badala ya kuliweka mabegani mwa Walawi, walibebe; wakaliweka juu ya gari libebwe. Wakachafua yote!

¹²⁶ Unaona, usipoenenda kulingana na ma—mapenzi ya Mungu, na njia ambayo Mungu ametuandalia kuiendea, daima wao hulichafua na kulibeba katika mashirika fulani, madhehebu, ujumbe fulani, na unaenda pale. Waona? Imefanywa hivyo daima.

¹²⁷ Jambo lilo hilo ndilo huyu kijana alilokabiliwa nalo. Alikuwa; alikuwa mfuasi wa—wa—labda Mafarisayo ama Masadukayo, ama shirika kubwa la siku hizo. Yeye alikuwa wa kidini kupindukia. Akasema, “Nimetii amri hizi nilizofunzwa, tangu utotoni.” Waona? Naye Yesu akampenda kwa ajili yake. Bali akakataa kuongozwa, akakataa kukubali uongozi halisi wa Yesu Kristo kumpa Uzima wa Milele.

¹²⁸ Tazameni, yeye aliamini kulikuwa na kitu tofauti na alichokuwa nacho ama hangalisema kamwe, “Mwalimu Mwema, nifanye nini sasa?”

¹²⁹ Mwaona, alitaka kufanya kitu fulani yeye mwenyewe. Hivyo ndivyo tunavyofanya, tunataka kufanya jambo fulani sisi wenyewe. Kipawa cha Mungu ni cha bure. Mungu hukupa wewe, hufanyi jambo lo lote Kwake. Yeye alikiagiza kwako, na utakipata. Waona?

¹³⁰ Tazameni, alijua kilikuweco. Alikiamini na alikitaka. Bali alipokabiliwa na yaliyompasa kutenda, hiyo ilikuwa tofauti na kanuni zake. Ilikuwa tofauti. Yeye angalishikilia fedha zake na kuwa mfuasi wa kanisa alilokuwa mfuasi wake, na kadhalika. Bali Yesu alijua hayo, na alijua alikuwa ameweka akiba fedha hizi, basi Yeye akasema, “Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, ukawape maskini. Kisha jitwike msalaba wako unifuata, nawe utakuwa na hazina Mbinguni.” Bali yeye hangalifanya hayo.

¹³¹ Wale viongozi wengine aliokuwa nao katika siku za ujana wake, walikuwa na ushawishi mwingi sana kwake hata yeye akakataa kukubali njia iliyoandaliwa na Mungu, ambayo ilikuwa Yesu Kristo; Yeye Yule tu aliye na Uzima wa Milele, Yeye Yule anayeweza kukupa wewe. Si kanisa, haliwezi kukupa Uzima wa Milele; hata jirani yako; hata mchungaji wako; hata kasisi wako; hata kanuni zako za imani; ni Yesu Kristo tu Mwenyewe anayeweza kukupa Uzima wa Milele.

¹³² Haidhuru wewe ni mwema vipi, yale umeacha kufanya, yale unayoanza kufanya, huna budi kukubali *Utu* wa Bwana Yesu Kristo. Ndiposa unapofanya hivyo, Yeye ni Neno, basi maisha yako yanalingana moja kwa moja na Neno na linajidhihirisha katika wakati huu unamoishi.

¹³³ Ilimpasa Nuhu kufanya hivyo kusudi Neno lidhihirike katika wakati wake. Naam, ingekuwa vipi kama Musa alikuja, kasema, “Tulijua aliyotenda Nuhu, tutachukua Neno la Nuhu. Tutatenda kama tu alivyotenda Nuhu. Tutajenga sa—safina na kueleza katika Mto Nile, na tuondoke Misri?” Naam, haingalifaulu. Mwaona, huo ulikuwa wakati mwingine.

¹³⁴ Yesu hangalikuja na ujumbe wa Musa; Luther hangalikuja na ujumbe wa Katoliki, Wesley hangalikuja na ujumbe wa Luther; Pentekoste haingalikuja na ujumbe wa Wesley. Wala Bibi-arusi hawezi kuundwa katika dhehebu la Kipentekoste, haliwezi kufanya hivyo. Na hiyo ni kweli kabisa. Limekwisha kufanyika dhehebu na likaenda humu, nalo ndilo hilo pale, kama tu yale mengine yao. Ni kapi. Kama tu uhai unavyopitia kwa . . . Mwaona?

¹³⁵ Huyo mwandishi, kama nilivyonena usiku uliopita, huyo mwandishi aliyekiandika hiki kitabu . . . Wala si kwa sababu alinilaumu vibaya sana, kasema eti nilikuwa “Ibilisi, iwapo kulikuweco kitu kama hicho.” Kwa hivyo yeye alisema hakumwamini Mungu. Akasema, “Mungu ambaye angekunja mikono Yake na kuketi kitako na kuwatazama hao wafia imani kote katika nyakati za kwanza, na adai ana uwezo wa kufungua Bahari ya Shamu, na kuwaachilia hao wanawake na watoto wararuliwe na simba na kadhalika, kisha akasema Yeye alikuwa Mungu Mwenye upendo.” Kasema, “Hamna kiumbe kama hicho.” Mnaona, mtu huyo, bila kutiwa pumzi kwa Neno hukosa kuliona.

¹³⁶ Ile punje ya kwanza ya ngano, Bibi-arusi, ilipaswa kuanguka ardhini kusudi ipate kuinuka tena. Vivyo hivyo yule Bibi-arusi wa kwanza aliyezaliwa katika Pentekoste ilimbidi kupitia katika Wakati huo wa Giza kama mbegu nyingine yo yote, apate kuzikwa. Walipaswa kufa. Hawana budi kufanya hivyo. Bali ikaanza kuchipuka tena katika Luther, katika yale marekebisha ya kwanza. Hayakuonekana kama mbegu iliopandwa, bali yalikuwa ndiyo Nuru ya wakati huo. Ule...?...ubua basi ukastawi hata ukaingia kwenye kishada, Wesley. Na kutoka kwenye kishada ukaingia katika Pentekoste, lile kapi.

¹³⁷ Unapotazama ngano, inapochipuka, punje ya ngano, mtu ambaye amelima ngano, nenda katazame umbo la hiyo ngano iliyomo humo, inaonekana hasa kama ile punje. Bali ukichukua koleo na ukaketi chini ukachukua hiyo ngano na kuifungua, hamna punje mle hata kidogo. Ni kapi tu. Nini basi nini? Li-limeumbika pale kushikilia punje. Mwaona? Ndiposa, muda si muda, uhai uliondoka kwe—kwe—kwenye ubua na kuingia katika kishada, kutoka kwenye kishada ukaingia kwenye kapi; unaacha kapi na kuingia kwenye ngano. Hatua tatu, mwaona, zake. Kisha unafanyika Ngano *nje* ya zile hatua tatu (Luther, Wesley, Pentekoste). Vivyo hasa. Mwaona, hapana shaka. Hauwezi kukatiza maumbile.

¹³⁸ Sasa tazameni, kila baada ya miaka mitatu baada ya ujumbe kutokea uliotumwa na Mungu, wao huunda dhehebu. Huu umekuweko kwa miaka ishirini, na hamna dhehebu. Halitakuweko. Mwaona? Sasa kapi halina budi kuondoka, kuipa Ngano nafasi ya kujilaza mbele ya Mwana ipate kuivishwa na Ujumbe, ikarudi moja kwa moja Kanisani tena, ikiunda Mwili wa Yesu Kristo kama tu ule wa Kwanza wa asili ulioingia ardhini. Sasa, kuona U—Uzima wa Milele.

¹³⁹ Uhai, hakika u—ubua humu nyuma ulibeba Uhai. Bila shaka, ulifanya hivyo. Bali, mwaona, ulipokuwa ubua na ukamalizika, lile dhehebu, ule Uhai ukasonga mbele moja kwa moja hata kwa Wesley; ukaondoka moja kwa moja. Kwani, . . . Hebu ukatazame kila moja wao. Naam, jani hilo kubwa linaonekana kama ile punje. Bali mbelewele ndogo inapokuja, kama . . . kwenye ka—kapi . . . ama ubua, mbelewele ya kishada, inaonekana sana kama punje. Bali inapofikia hilo kapi, ni kama iko pale.

¹⁴⁰ Je, Yesu hakusema, “Katika siku za mwisho” (Mathayo 24:24) “zote mbili zitafanana sana hata ingeipoteza ile chembechembe hai yenyewe, yule aliye Mteule, aliyechaguliwa tangu awali, kama yamkini?” Karibu sana na iliyo ya kweli, mwaona. Kwa hivyo, katika siku za mwisho. Basi, mnaona, ni wakati wa ngano sasa. Inafikia wakati wa mavuno. Huu sio wakati wa Luther, huu si wakati wa Pentekoste, huu ni wakati wa Bibi-arusi.

¹⁴¹ Kama Musa alivyoliita taifa toka kwa taifa, Kristo leo analiita Kanisa toka kanisani, mnaona; jambo lile lile katika mfano, akiwapeleka kwenye Nchi ya Milele Iliyoahidiwa, iliyo tukufu.

¹⁴² Basi kumkataa huyo Mtu anayeitana, Kristo, haidhuru kama wewe ni Mpetekoste, Mmethodisti, Luther, hata uwe nani, inakupasa. . . Wakati huu! Sina neno dhidi yao, hata kidogo, bali katika wakati huu *sasa* huna budi kuukubali (kama walivyofanya katika wakati huo) Utu wa Kristo ambao ni Neno!

Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.

Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; . . .

. . . yeye yule jana. . . leo, na hata milele (Waebrania 13:18)

Waona, huna budi kumkubali huyo Mtu wa Uzima wa Milele!

¹⁴³ Sasa, Uhai aliokuwa nao Luther, ulikuwa kuhesabiwa haki, Wesley alikuwa na kutakaswa, alikoongezewa. Pentekoste ilikuwa na kurudishwa kwa zile karama, zilizoongezwa kwake. Bali sasa ni kukamilishwa kwa mwili, mwaona, zile sehemu tatu zake, na kutoka kwa hizo. . . Sasa, ufufuo utakapokuja, ule uhai ulioishi katika hao Walutheri, ulioondoka, uhai ulioishi katika Wamethodisti na ukatoka, ule uhai ulioingia kwa Wapetekoste, utanyakuliwa wote kutoka ardhini katika Mwili wa Bibi-Arusi kupelekwa mbele ya Yesu Kristo. Mungu atukuzwe! Jamani, inawasha moyo! Ni Kweli!

¹⁴⁴ Tumepiga kona! Tunatazama Mbinguni, tukungoja kule kuja; kile Kifuniko cha Piramidi, tuseme, kule kurudi Kwake! Kanisa halina budi kufufuliwa hivi karibuni, na hatuna budi kujiweka tayari.

¹⁴⁵ Na njia pekee uwezayo, si kusema, “Vema, mimi ni mshiriki wa Assemblies. Ni mshiriki wa Umoja, Uwili,” ama cho chote kile, yote pale, “Mimi ni mshiriki wa Church of God,” hilo halimaanishi cho chote. “Baba zetu walipaza sauti na kurukaruka,” hiyo ni barabara kabisa, hiyo ilikuwa siku *yao*. Bali *leo* umekabiliwa si na dhehebu walilounda, bali na Uzima unaoendelea, ambao ni Yesu Kristo.

¹⁴⁶ Huyu kijana alikuwa ametenda jambo lile lile. Musa aliandika hizo amri. Bali, mwaona, Mungu yule yule aliyeandika hizo amri kwa nabii Wake, ndiye yule yule aliyetabiri ya kwamba siku ingekuja, “Nitawainulieni Nabii aliye kama mimi. Na itakuwa ya kwamba wote ambao hawatamsikia Yeye watakatiliwa mbali”; kule nyuma kwenye makapi ya kidhehebu pamoja na vishada. Hawana budi kufikia Uzimani. Na leo, usije ukasema, “Mimi ni Mpetekoste. Mimi ni mfuasi wa *hili*, ni mfuasi wa *lile*” Hilo halimaanishi cho chote. Huna budi kuukubali Utu

wa Kristo, Uzima wa Milele. Inatukabili kila mmoja wetu! Usije ukasahau hilo.

¹⁴⁷ Kuna viongozi, mwaona, waliomshikilia sana, hao watu waliosema, “Vema, sisi ni wafuasi wa *hili*, na tu wa *lile*,” nao wakamshikilia sana. Bali ni jambo baya vipi kukataa uongozi wa Uzima wa Milele!

¹⁴⁸ Naam, Uzima huo umo hapa usiku wa leo. Hiyo ni kweli. Roho Mtakatifu yuko hapa, ambaye ni Kristo katika umbo la Roho; Roho Wake, upako uko hapa.

. . . Kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, bali ninyi mtaniona . . .

. . . Kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata utimilifu, hata ukamilifu wa dahari.

¹⁴⁹ Yesu peke Yake ndiye anayeweza kukuongoza hata kwa huo Uzima wa Milele. Hamna kanisa, hamna dhehebu, hamna mhubiri, hamna kasisi, hamna kingine cho chote kinachoweza kukuongoza Kwake, kuna budi kuongozwa Naye, Ndiye tu anayeweza kukuongoza.

¹⁵⁰ Je, ungaliwazia Yeye akikuongoza nje ya Neno Lake, ambalo ni Yeye? Na iwapo Yeye ni Neno, nawe u sehemu Yake je, wewe hutakuwa sehemu ya Neno? Neno ambalo Mungu anataka kumwagilia maji ya wokovu leo, kumtambulisha Yeye leo; kama mitume walivyomtambua Yeye, kama Luther, kama Wesley, kama watu siku hizo walivyomtambua Yeye. Hizi ni nyakati zingine. Ni Neno! Neno lilisema mambo haya tunayoyaona yakitendeka sasa, yamebashiriwa kutendeka katika majira haya. Kwa hivyo mkubali Yesu Kristo na umwache akuongoze hata kwenye Uzima wa Milele.

¹⁵¹ Ingawa alikuwa amefanikiwa, huyu kijana . . . Yeye alikuwa amefanikishwa mambo yote mazuri. Shuleni, alikuwa mzuri. Kama kijana mzuri, hapana shaka, yeye alikuwa mzuri. Kama baba halisi . . . katika kumsikiza babaye katika biashara, yeye alikuwa kijana m—mzuri. Mwema kwa wazazi wake. Alikuwa mtiifu kwa kasisi wake. Alikuwa mwaminifu kwa kanisa lake. Alikuwa mwaminifu kwa amri za Mungu. Bali akapoteza kitu muhimu sana, na vingine nyote hivikuwa vya maana sana kwake alipoupuuzwa uongozi wa Uzima wa Milele, Yesu Kristo.

¹⁵² Tazameni! Uongozi huu unamkabili kila mmoja wetu leo, jambo lile lile lililomkabili huyo kijana, sisi . . . haidhuru sisi ni wa kidini vipi. Huenda ukawa Mkatoliki, huenda ukawa Mbatisti, Mmethodisti, ama huenda ukawa Mpetekoste, ama cho chote ulicho, jambo lili hili linakukabili usiku wa leo: Uzima wa Milele, hiyo ni, kumkubali Yesu Kristo. Tumepewa nafasi hii.

¹⁵³ Wakati mwingine maishani hatuna budi kukabili jambo lilo hilo kama alivyofanya huyu kijana, kwa maana wewe ni mwanadamu na umepewa—umepewa nafasi ya chaguo. Una

chaguo. Mungu aliifanya hivyo upate kuchagua. Kama aliwapa Adamu na Hawa hiari ya kukata shauri iii wapate kuchagua nao basi, wakachagua vibaya. Na mnaona, Yeye hawezi kuwafanyia zaidi ya alivyowafanyia wao, hana budi kuwaweka katika hali ile ile ili tupate kuchagua ama kukataa.

Mna chaguo. Hebu tuchunguze baadhi yao:

154 Una chaguo, kama kijana, iwapo utapata elimu au la. Una chaguo hilo. Unaweza kutaka kuwa “asiye nayo,” unaweza tu kuikataa.

155 Una chaguo la mwenendo wako. Nitaumiza kidogo hapa. Mwaona? Unaweza kuondoka ukaachilie nywele zako zikue na uwe beatle ama mmoja wa hawa majuha.

156 Ama ninyi wanawake, mnaweza kuonekana kama wanadamu wenye heshima ama mnaweza kuwa mmoja wa hawa viumbe wa kishetani tulio nao hapa, hayo macho ya buluu. Na huu mtindo wa kukata nywele na kadhalika, hayo ni kinyume cha Neno la Mungu kabisa, ambayo hayapatani nalo kabisa; hata haungeomba . . . haungesali na hayo maombi yakubalike. Hiyo ni Kweli. Kweli kabisa. Hivyo ndivyo Biblia ilisema.

157 Lakini ni nini kimetukia kwenu, kanisa? Mmeona televisheni kwa wingi sana, mambo mengi sana ya ulimwengu, ni rahisi sana kwa ile tabia yenu ya kale ya Adamu kuingilia hayo, kutenda kama wengine wao.

158 Hebu nirudie hili tena! Katika ule mkate usiotiwa chachu, katika kule kutolewa kwa—kwa—upatanisho katika siku za Musa, Musa alipowatoa wale wana, ilipaswa kuwe na siku saba ambapo hapakuwepo chachu kati ya watu. Kila mtu ajua hilo. Katika Kutoka, “Kusionekana chachu hata kidogo kambini mwenu, siku saba.” Hizo *siku saba* ziliwakilisha zile “yakati zote saba za kanisa.” Mnaona?

159 “Kusiweko chachu.” Sasa, hiyo ni nini? Kusiweko na kanuni za imani, kusiweko dunia, Yesu alisema, “Mkiipenda dunia wala mambo yaliyomo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yenu.” Mnaona? Nasi tunajaribu kuchanganya hayo; hauwezi kufanya hivyo! Inakupasa kufikia jambo *moja* kuamini: au utamwamini Mungu, au utaamini kanisa lako, utaamini dunia. Hu—huwezi kuichanganya pamoja. Na hauwezi kushikilia hayo mambo ya kale ambayo kanisa lililokutangulia liliyashikilia. Huna budi kuuchukua Ujumbe na majira yake.

160 Yeye alisema, “Kitakachosalia, usikiache hata asubuhi (kufikia wakati huu mwingine), kiteketeze kwa moto; kiangamizwe.” Ya kwamba wakati unaoishi, Ujumbe wa wakati huu, hauna budi kutolewa Maandikoni na kuthibitishwa na kuhakikishwa na Mungu ya kwamba ni Mungu anayetenda hivyo. Ndiposa utaupokea Huo au utaukataa. Huo ndio Uzima wa Milele, uongozi wa Roho Mtakatifu, akiongoza Kanisa Lake.

161 Tungedumu kwa hilo muda mrefu, bali hebu tusonge mbele, tuendeleo kusonga mbele tu.

162 Chaguo la mwenendo wako. Wewe... Hauwezi kuichanganya sasa. Uko upande wa Mungu au dhidi ya Mungu, na unachotenda nje huonyesha kilicho ndani. Waona? Gugu, sisi kuwazia tu, “Nina ubatizo wa Roho Mtakatifu, ninaenda Mbinguni.” Hiyo haimaanishi jambo hata moja eti unaenda Mbinguni. La, bwana. Unaweza kupata ubatizo wa Roho Mtakatifu kila saa maishani mwako, na hata hivyo upotee na kwenda jehanamu. Biblia inasema hivyo. A-haa, hiyo ni kweli hasa.

163 Tazama hapa, wewe ni mtu wa nje. Una hisi tano ambazo zinawasiliana na huo mwili wa nje. Mungu alikupa hisi tano, si kuwasiliana Naye, mwili wako wa duniani: kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia.

164 Kisha una roho ndani yake, nayo ina hisi tano: dhamiri, upendo, na kadhalika. Njia tano ambazo unawasiliana na ulimwengu wa roho kwazo, bali kwa roho yako.

165 Mwili wako huwasiliana na vitu vinavyoonekana. Roho yako huwasiliana na vitu vya kiroho. Bali ndani yake una nafsi, na hiyo nafsi ndiyo ile chembechembe hai inayotoka kwa Mungu.

166 Na kama mtoto mchanga aliyeumbika tumboni mwa mamaye. Mtoto anapoingia tu—tumboni mwa mamaye, ile chembechembe dogo, inatambaa hata kwenye yai. Haifanyi chembechembe moja mwanadamu, nyingine mbwa, na nyingine paka, na nyingine farasi. Zote ni chembechembe za binadamu kwa sababu zinafanyika kutoka chembechembe yenye asili ya binadamu.

167 Na mtu anapozaliwa mara ya pili na Neno la Mungu, akachaguliwa tangu awali Uzima wa Milele, akaitwa “Aliye Mteule,” itakuwa Neno la Mungu juu ya Neno, Neno kwa Neno! Si kanuni za imani za kidhehebu kisha Neno, na kanuni ya imani; nayo haiwezekani. Hauwezi kuwa na hiyo chachu ndani yake! Mna Uzima wa Milele mmoja tu, Yesu Kristo aliye Neno:

Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.

Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu. . .

168 Marafiki, ninyi huwalisha watoto wangu. Mnanituma kufanya kati ya umishenari ulimwenguni, kupeleka Ujumbe. Sina budi kuwa mwaminifu kwenu Yale ninayotazama, labda ninyi hamyaoni. Hiyo ndiyo sababu niko hapa, kujaribu kuwaambienu. Si kwa sababu siwapendi watu, ni kwa sababu nawapenda watu. Kuwasahihisha. Ninapoona kuteleza kwa kanisa, wakiondoka huku wanasema, “Vema, tulifanya hivi na tulifanya vile,” na kutazama kanisani na kuona...Haitafaa kitu.

169 Kisha natazama hapa katika Biblia na kuona haina budi kuwa hivyo wakati wa mwisho, huo Wakati wenye uvuguvugu wa Kanisa la Laodikia, wakimfukuza Yesu nje (Neno). Yeye hakuita kamwe. . . Yeye hataita kanisa lo lote. Yeye alisema, “Wote niwapendao Mimi nawakemea. Nawarudi.” Nilichukua Neno na kulisisitiza, nikiwaambieni, “Mmelikosea!” Hiyo ndiyo sababu mimi nawapenda. “Iwapo mtafungua mlango niingie, nitakuja na kula pamoja nanyi.” Si kanisa, Yeye tayari amefukuzwa kwakwe.

170 Linaelekea kwenye Baraza la Ekumenia. Huko ndiko limekwisha kwenda moja kwa moja kurudi Rumi lilikotoka. Na hiyo ni kweli hasa. Niliandika hayo kijikaratasi ni miaka ishirini na mitano iliyopita, ama maiaka thelathini na mitatu iliyopita, na ndiyo hayo. Isitoshe, imeandikwa katika Biblia, kuhusu maono. Limerudi. Hamna njia ya kuliokoa, limekwisha! Itakuwa hivyo.

171 Mungu anaita *watu binafsi*. “Nasimama mlangoni, nabisha. Kama mtu awaye yote, mtu ye yote. . .” Mtu mmoja binafsi kati ya elfu moja, huenda ikawa mmoja kati ya milioni moja.

172 Kama nilivyosema siku chache zilizopita. Israeli ilipotoka Misri, kulikuweco na watu wapatao milioni mbili waliokuja, na yapata milioni mbili tu; mmoja tu. . . ni watu wawili tu walioingia. Mmoja katika ya milioni moja. Je, ulijua hilo? Kalebu na Yoshua.

173 Na Yesu, alipokuwa duniani. Wao walisema, “Baba zetu walikula mana jangwani. Sisi tunafuata hayo mapokeo. Pia tunafanya *haya*. Tunajua mahali tunaposimama!”

174 Yeye akasema, “Najua baba zenu walikula mana jangwani, nao wametenganishwa Milele. Wamekufa!”

175 Shahawa zinapotoka kwa mwanamume au mwanamke, mna mayai milioni moja yanayotolewa, mna chembechembe hai milioni moja zinazotoka. Na kutoka kwa hizo chembechembe zote hai na dogo, za aina. . . Iwapo ni—iwapo ni za dume, ama mwanamume, ama cho chote kile, mna chembechembe hai milioni kadha, chembechembe milioni zikitenda kazi. Mle mna chembechembe moyari tu iliyokusudiwa uhai, kwa maana mna yai moja mle, lililo tayari, kukutana nayo. Hiyo ni kweli. Itakutana na yai moja tu. Kama tu mwili huu unaoketi hapa, nayo chembechembe hai hutoka kwa Mungu. Mwaona? Basi tazama chembechembe hiyo dogo hai ikija kutoka kwa chembechembe hizi zingine zote, na kujongea karibu nazo, ikazipita, ikaja hapa na kupata hilo yai lililo tayari na—na kuliingiza ndani; na zile zingine zinakufa.

176 Vipi kama ingalikuwa hivyo kwa kanisa leo, mmoja kati ya milioni? Waona mahali ingekuwa? “Mlango ni mwembamba, na Njia imesonga, nao waionayo ni wachache; maana njia ni pana iendayo upotevuni, na kutakuwa na wengi watakaoiendea.” Hiyo

ni kweli, Ndugu Branham? Sijui, bali ninanukuu tu Maandiko. Mwaona?

¹⁷⁷ Sasa, umeagiziwa Uzima. Utauona iwapo umeagiziwa kuuona. Iwapo hukuagiziwa kuuona, hautaona. Kasema, “Wana macho bali hawawezi kuona, maskio na hawasikii.” Jinsi mpaswavyo kuwa na shukrani, kanisa! Jinsi iwapasavyo kujinyosha wenyewe toka kwa mambo haya! Jinsi iwapasavyo kuwa na juhudi kwa Mungu! Kwamba macho yenu yanaona mnayoona, na maskio yenu yanasikia mambo mnayoona. Uongozi! Mbona mkaja humu usiku wa leo kusikia ujumbe kama HUU? Ninaitwa ulimwenguni kote, na makanisa, “mshupavu wa dini.” Mbona mkaja? Roho Mtakatifu aliwaongoza humu (mwaona? mwaona?) kusikiza. Tahirini. Katilieni mbali mambo yenu ya ulimwengu, kubalini uongozi wa Yesu Kristo, la sivyo, mtaangamia bila shaka kama ulimwengu.

¹⁷⁸ Una chaguo la mwenendo. Jinsi unavyoenenda, hiyo ni shauri lako.

¹⁷⁹ Una chaguo la mke. Unaondoka na kuoja mke wako. Ukitaka kuoja mke, unataka kuoja yule anayeambatana na... jinsi unavyotaka... unavyopanga nyumba yako ya usoni iwe. Je, ungewazia mwanamume, mwanamume Mkristo, akiondoka na kutwaa mmoja wa hawa Vipusa wa kisasa kama mke? Waona? Ungewazia hayo? Je, mtu huyo anafikiri nini? Atakuwa na nyumba ya namna gani kama akichukua mwenda uchi, mcheshi mwigizaji kutoka barabarani hapa, kahaba wa barabarani? “Lo,” mnasema, “sasa, ngoja kidogo.” Je, anajivalishaje? Mwaona? Mwaona? Kuvaa suruali fupi na kadhalika, yeye ni kahaba wa barabarani. “Lo,” mnasema, “sasa, Ndugu Branham!” Jamani, maskini rinda hizo zenye kubana, yaonekana kama kwamba umemwagiliwa mle, kahaba wa barabarani.

¹⁸⁰ Yesu alisema, “Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Basi hana budi kuhukumiwa kwa ajili ya hilo. Naye alifanyaje? Alijionyesha mwenyewe. Ni nani aliye na hatia? Wazia hilo.

¹⁸¹ Unasema, “Hawatengenezi nguo zingine.” Wana majora na cherahani. Mwaona, hamna udhuru. A-haa. Hiyo ni kweli hasa.

¹⁸² Basi, sitaki kuwaudhi. Na huu si mzaha, hii ni BWANA ASEMA HIVI kutoka Maandikoni. Ni kweli hasa, marafiki. Mimi ni mzee, sina muda mwingi wa kuishi, bali sina budi kuwaambieni yaliyo Kweli. Iwapo huu ndio ujumbe wangu wa mwisho, ni Kweli. Mwaona? Usifanye hivyo, dada. Usifanye hivyo, ndugu.

¹⁸³ Nanyi watu mnaoshikilia ka-kanuni za imani, huku mkijua Neno la Mungu tayari limethibitishwa mbele zenu. Ubatizo wa Roho Mtakatifu na mambo haya yakini tuliyo nayo siku hizi, halafu, kwa sababu ya kanuni zenu za imani, mnayapa

kisogo? Je, unawezaje kuwa mwana wa Mungu na ulikane Neno la Mungu lililobashiriwa kwa siku hizi za mwisho tunazoishi? Mnawezaje kufanya hivyo? Biblia yawezaje kuliita hili . . . ?

¹⁸⁴ Kama nilivyosema usiku uliopita kuhusu m—mfalme wakati mmoja, kule kusini, walipokuwa . . . yule mtu mweusi aliuzwa kama mtumwa. Naam, hawakuwa bora kuliko so—soko la motokaa zilizotumiwa, wamebandikwa bei juu yao. Nami nilishtushwa na mahali padogo . . . Nalisoma siku moja ambapo dalali alikuja kununua baadhi yao naye akasema, “Vema, sasa, ningetaka . . .” Wao walikuwa na huzuni, ingalikubidi kuwapiga mijeledi, kuwafanya wafanye kazi kwa sababu walikuwa mbali na nyumbani. Walikuwa wameuzwa, watumwa. Nao wakiwa katika nchi ya kigeni wasiyojua kamwe, nao hawangalirudi nyumbani kwao tena, nao waliona huzuni. Ilikubidi kuwapiga mijeledi, kuwafanya wafanye kazi. Bali huyu dalali akafika kwenye shamba moja.

¹⁸⁵ Kijana mmoja pale kifua nje, kidevu chache juu, haikumlazimu kumpiga mijeledi. Yeye alikuwa amechangamka sana, naye akawatia moyo wale wengine.

Huyo dalali akasema, “Nitamnunua.”

¹⁸⁶ Yeye akasema, “Hauzwi. Simuuzi. Hutamnunua, maana hauzwi.”

¹⁸⁷ Akasema, “Vema, nini kinachomfanya tofauti hivi?” Akasema, “Je, yeye ni kiongozi wa hao wengine?”

Kasema, “La.”

Kasema, “Unamlisha tofauti?”

¹⁸⁸ Kasema, “La. Naam, yeye ni mtumwa, yeye hula mle siniani pamoja na wale wengine.”

Kasema, “Nini kinachomfanya tofauti hivyo?”

¹⁸⁹ Yeye akasema “Nalishangaa mimi mwenyewe, hata nilipotambua. Kule Afrika (walikotoka, ambako Makaburu waliwanunua, na kuwaleta hapa na kuwauza kama watumwa), kule babaye ni mfalme wa hilo kabila. Hata hivyo, akiwa mgeni, mbali na nyumbani, yeye anajua ya kwamba yeye ni mwana wa mfalme. Kwa hivyo yeye hujichukua hivyo.”

¹⁹⁰ Ni karipio jinsi gani kwa Ukristo! Tunatazamiwa kumwakilisha Mungu na Uzima wa Milele. Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na hiyo ni Mungu. Yeye pekee ndiye aliye na Uzima wa Milele. Nasi tumetokana Naye, kwa maana sisi ni chembechembe za Roho Yake. Basi yatupasa kuwa na mwenendo wenyewe, wanawake kwa wanaume, kama Biblia ilivyotuambia kutenda. Si Mayezebeli wa barabarani, na walaghai wa madhehebu; bali Wakristo waungwana, wana wa kiume na wa kike wa Mungu, waliozaliwa kwa Roho wa Mungu, wakidhihirisha Nuru katika siku zetu na kuitawanya. Hiyo ni kweli hasa.

191 Lakini jinsi tumechukuliwa kutoka kwake! Kwa nini? Jambo lile lile huyu kijana alilotenda hapa. Alikataa, alikataa Uzima wa Milele, kwa sababu ungemgharimu cheo chake, ungemgharimu anasa za—za—zake za kifedha, ungemgharimu ushirika wake kanisani, ungemgharimu mambo mengi sana. Alijua yale ungemgharimu, yeye alikuwa kijana mwenye busara, naye alijisikia ya kwamba hangelipa gharama hiyo. Hata hivyo, aliwaza, “Mimi nitaitumaini tu dini yangu na kuendelea.” Bali moyoni mwake alijua kulikuweco jambo fulani kuhusu Yesu Kristo lililokuwa tofauti na hao makuhani wa siku hizo.

192 Na Ujumbe wo wote ujao, Ujumbe halisi uliozaliwa na Mungu, ni tofauti na mwenendo wa kizamani. Uponyaji wa Kiungu ulipoanzishwa, si muda mrefu umepita, je, mlitambua jinsi waigaji waliufuata? Mnaona? Na kila mmoja wao akaingia moja kwa moja katika madhehebu hayo, akadumu humo. Je, kuna anayejua ya kwamba kulipaswa kuwe na Ujumbe kufuata huo? Naam, Mungu hatufurahishi! Yeye huvutia usikivu wetu kwa jambo fulani, na anapovuta usikivu wetu, basi Yeye yuna Ujumbe Wake.

193 Tazama alipokuja duniani mara ya kwanza na akaanza huduma Yake, “Ee, Rabi kijana, tunakutaka humu kanisani mwetu. Tunaweza . . . Shuka uje huku.” Yule nabii kijana. “Lo, tunakutaka huku. Njoo huku.”

194 Bali siku moja Yeye akasimama na kusema, “Mimi na Baba yangu tu Mmoja.”

195 “Lo, jamani! Anajifanya mwenyewe Mungu.”

196 “Msipoula Mwili Wake Mwana wa Adamu na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani Yenu.”

197 “Yeye ni kizuu kifyoza damu! Vema, hatuhusiani na hayo.”

198 Hao mitume wakaketi papo hapo: maelfu wakamwacha, bali hao mitume walikuwa wamekusudiwa Uzima. Yeye alisema hivyo. Hawangaliweza kuyaeleza. Waliamini. Walidumu nayo kwa sababu, walisema, “Hamna mtu angaliweza kutenda kazi hizi.”

199 Hata makuhani walijua hivyo. Nikodemo alisema, “Tunajua” (lile Baraza la Kiyahudi) “ya kwamba hakuna mtu angaliweza kuzifanya kazi hizi isipokuwa zimetoka kwa Mungu.” Mwaona?

200 Petro, kwenye Siku ya Pentekoste, alisema, “Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa na Mungu kati yenu. Mungu alikuwa pamoja Naye.”

201 Tazama katika Maandiko, kile Maandiko yalisema afanye. Yesu alisema, “Mwayachunguza Maandiko, mnadhani ya kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani yake. Hayo ndiyo yanayonishuhudia. Mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi, kwa maana Musa aliandika ya kwamba ningekuja, katika umbo

ambalo ningalikuja kwalo.” Yeye alikuja kama Mwana wa Adamu.

²⁰² Yeye yuaja katika majina matatu, kama Mungu. Matatu (kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu), Mungu yule yule, ni sifa tatu.

²⁰³ Haya basi, pia, kuhesabiwa haki, kutakaswa . . . ; Luther, Martin, na—na—Pentekoste; jambo lile lile: sifa tatu, sehemu tatu, nyakati tatu za kanisa.

²⁰⁴ Jambo lile lile: maji, damu na roho. Daima unapo-unaposonga mbele, vitu vitatu vinavyokurudisha mwilini. Kama vile inavyokuleta kutoka uzazi wako wa kawaida, inaonyesha uzazi wako wa kiroho kwa mfano. Mtoto mchanga anapozaliwa, jambo la kwanza ni maji, yakifuatiwa na damu, kisha uhai. Hiyvo ndivyo ulivyoingia katika Ufalme wa Mungu, vivyo hivyo. Waona? Ndivyo Kanisa linavyoingia, vivyo hivyo. Jambo lile lile. Sasa tazama mambo haya matatu, Mungu amefanya . . . anaumba mwili Wake.

²⁰⁵ Sasa tunaona ya kwamba humu ndani, ya kwamba una haki ya kujichagulia. Unamchagua msichana unayetaka kumwoa; yeye akikubali, vema.

²⁰⁶ Kisha jambo jingine, una chaguo iwapo unataka kuishi ama hutaki kuishi. Unachagua leo kati ya Uzima na mauti. Unaweza kuishi.

²⁰⁷ Huyu kijana alikuwa na chaguo hilo. Yeye alifaulu katika mambo mengine yote, mtu wa kidini, bali alijua wakati huyo . . . Yeye alinena juu yake mwenyewe. “Nimezishika amri hizi tangu utoto wangu,” bali alijua hakuwa na Uzima wa Milele. Mwaona? Naye alikuwa na chaguo kuupokea ama kuukataa, naye akaukataa. Hilo lilikuwa kosa baya sana angaliweza kufanya. Yale mengine hayangalifaa kitu. Hayafai, hayafai kitu, isipokuwa ufanye chaguo Hilo.

²⁰⁸ Hebu sasa tumfuatilie katika chaguo lake, tukaone lilikomwongoza. Sasa, oneni alikochagua. Naam, tazama, yeye alikuwa—alikuwa mtu tajiri, alikuwa mfanyi biashara, alikuwa mtawala, naye alikuwa mtu wa kidini. Yote hayo!

²⁰⁹ Siku hizi tungesema, “Jamani, yeye ni Methodisti halisi, Mbatisti ama Mpetekoste. Yeye—yeye ni mtu kweli kweli, mvulana mzuri sana. Mzuri!” Hungalisema neno juu yake; mpole, mwema, mpenda watu na kila kitu. Hana utovu wa uadilifu. Huenda ikawa hakuvuta sigara, hakunywa pombe ama kutangatanga kwenye tamasha pamoja na dansi, vyo vyote tungeliviita siku hizi, jinsi tungelimfananisha Mkristo. Bali hivyo bado si Uzima wa Milele! Hayo siyo tunayonena habari zake. Huenda alikuwa mwaminifu kwa kanisa lake, ambamo alimokuwa labda. Lakini, mwaona, na hili lilimwongoza wapi? Kupendwa sana na watu wote. Tusema, kama alikuwa mhubiri, angalikuwa . . . angepata kanisa bora. Huenda angekuwa mzee

wa mkoa ama askofu. Mwaona? Inakuelekeza kupendwa na watu wote, na ilimwongoza katika utajiri na sifa.

²¹⁰ Huenda ikawa vivyo hivyo leo iwapo una majaliwa makubwa ya kuimba. Naliwazia yule kijana mwanamume aliyeuimba wimbo huo hapa muda mfupi uliopita; jinsi alivyompa Ibilisi hayo, na sasa ameyapata tena. . . Na jinsi alivyo tofauti na Elvis Presley na wengine wa hawa. Pat Boone, na kundi kama hilo, Ernie Ford, watu hao, waimbaji mashuhuri; na kuchukua majaliwa yao, majaliwa waliyopewa na Mungu, na kuyatumia kuendeleza ka—kazi ya Ibilisi. Hiyo ni kweli. Baadhi ya waimbaji mashuhuri wakiuza majaliwa waliyopewa na Mungu kwa ajili ya sifa katika ulimwengu huu, kuwa watu mashuhuri. Ungewezaje kuwa “maarufu” zaidi ya vile ungaliweza, kuwa mtu mashuhuri, kuliko kuwa mwana wa Mungu?

²¹¹ Sijali iwapo unamiliki mji mzima, dunia nzima, nawe hujakubali uongozi wa Uzima wa Milele kwa Roho Mtakatifu (Kristo), utawezaje. . . U nani wewe, hata hivyo? U mwanadamu aliyekufa, umekufa katika dhambi na makosa! Hata uwe wa kidini vipi; hata uwe mwaninifu vipi kwa kanisa; muhubiri, iwapo unataka kuwa mimbarani; bali kuukataa, unakufa!

²¹² Yeye alikuwa ameisha kufanikiwa sana. Alikuwa amefanikiwa sana katika maisha haya. Bila shaka. Tunamwona ambapo tunamkuta. . . Kisha tunaona mtu huyu, ya kwamba alienda. . . Tunamfuata kidogo, na tunaona amefanikiwa sana. Nasi tunamfuatilia kote katika Biblia. Tunaona ya kwamba ye—yeye. . . Tunamwona ni mtu tajiri. Ana manyumba makubwa sana, yeye alikuwa akiwakaribisha hakimu pamoja na meya wa jiji, ama ye yote yule. Yeye yumo juu ya dari yake, na ana karamu murua: na waandishi wa kike, na wanawake, wasichana, na kila kitu, karibu naye. Na kuna mwombaji mlangoni mwake, aliyelitwa Lazaro. Yeye anamfagilia makombo. Tunajua hadithi hiyo. Jambo lingine, yeye anaendelea kufanikiwa, kama makanisa siku hizi yavavyofanikiwa.

²¹³ Mfanyi biashara anayeketi hapa, ameniambia, “Papa hapa California, ya kwamba kanisa lapaswa kukiambia chama cha wafanyi kazi la kutenda.” Mwaona, imefikia kanisa na taifa tena. Kikulacho ki nguoni Mwako. Mnaona, mko pale ndani, na mtapokea alama ya myama bila kujua.

²¹⁴ Kama mliwahi kununua mojawapo ya kanda zangu, ipateni nitakapoipata, nitakapoenda nyumbani, *Ule Mkondo wa Nyoka*; na mtaona ilipo, mtaona hili linapoishia. Naenda nyumbani sasa kuuhubiri, Bwana akipenda. Itachukua yapata masaa manne, kwa hivyo singeweza kuiweka katika mmoja wa mkutano kama huu. Inanipasa kwenda kule ambako kanisa hunivumilia kwa muda mrefu sana, kwa uvumilivu. Tazameni, lakini sasa. . . Mnaweza kusikiza hiyo kanda wakati mwingine nyumbani mwenu.

215 Tazameni hili, sasa tunaona ya kwamba yeye alikuwa amefanikiwa sana. Kisha tunamwona baadaye alipokuwa amefanikiwa sana, hata akasema, “Nina mali nyingi sana!” Jamani, yeye angalikuwa mtu kwelikweli wa kisasa. Sivyo? “Hata ghala zangu zimejaa kanisa, nusura zipasuke. Nami nina mali nyingi sana hata nikasema, ‘Ee nafsi, starehe.’”

216 Lakini ni nini alichotenda hapo mwanzoni, yeye aliukataa uongozi wa Yesu Kristo. Kanisa lake, akili yake, elimu yake, na kadhalika, zilimuongoza kwa ufanisi. Wayahudi wote walimpenda. Yeye aliwapa vitu, aliwasaidia, huenda alitenda *hili, lile* au *lingine*. Bali, waona, yeye alikataa u—u—uongozi wa Yesu Kristo, Uzima wa Milele. Na huo. . . Biblia ilisema, Yeye alisema, “Mpumbavu wewe, usiku wa leo roho yako inatakiwa.”

217 Na sasa tunamwona (mahali pengine) katika jehanamu; akiinua macho yake na kumwona yule mwombaji, aliyemfukuza barabarani, kifuani mwa Ibrahimu. Ni kosa haya vipi! Jinsi makanisa ya—ya—ya—yalikuwa ajabu jinsi yalivyoenenda, bali hawakuwa na Uzima wa Milele.

218 Hilo linanikumbusha juu ya mahubiri niliyohubiri hapa si muda mrefu umepita, *Chujio la Mtu Mwenye Busara* Huenda mliipata. Nalikuwa nikienda, nikitembea mwituni, nilikuwa nikiwinda kindi (majira haya ya kupukutika kwa majani) nami nikaangalia chini. Na, bila shaka, siwezi kutaja kampuni hiyo ya sigara. Mnaijua. Na kulikuweco pale pa—pakiti ya sigara imeanguka pale. Nami nikaipita tu, nikitafuta. . . kule mwituni. Nami nikaona pakiti hiyo imelala pale, nami nikatazama nyuma, ilisema, “Chujio la mtu mwenye busara, ladha ya mtu anayevuta sigara.” Nikaanza kutembea mwituni.

219 Naye Roho Mtakatifu akasema, “Geuka ukaichukue.”

220 Nami nikainama nikaitwaa, “Chujio la mtu mwenye busara, ladha ya mtu anayevuta sigara.” Nikawaza “Kampuni ya Kiamerika hapa, inauza mauti kwa hila, kwa raia wao wa Amerika.” Chujio la mtu mwenye busara? Ninyi. . . Na ladha ya mtu anayevuta sigara?

221 Nilikuwa kwenye Maonyesho ya Ulimwengu, pamoja na Yul Bryan. . . Brynner, na wengineo kule, alipokuwa akifanya majaribio. Na jinsi aliweka sigara moja na kuvuta. . . kupitia kwenye marmar na kuchukua. . . Akapangusa sumu ya tumbako na kuingiza mgongoni mwa panya, panya mweupe, na katika muda wa siku saba alikuwa amejaa kansa hata hangaliweza kutembea. Nao wakasema, “Mwajua, wao husema ‘chujio,’” kasema, “ni hila, wanauza sigara nyingi zaidi.”

222 Inachukua sumu nyingi zaidi kumridhisha huyo pepo. Hiyo ni kweli. Na unapochukua sigara iliyo na chujio, inachukua kama sigara nne badala ya moja isiyo na chujio. Ni hila, kusudi wakuuzie sigara nyingi zaidi. Hauwezi kuwa na moshi usio na rami; nayo rami, inakupa kansa. Mwaona vile ilivyo? Nao

Waamerika vipofu, wakimtazamia sungura atoke kwenye kofia mahali fulani, wanadanganyika. Huwezi kuupata; ni mauti, sijali utaenda wapi, ni mauti ko kote uendako. “Chujio la mtu mwenye busara,” mtu mwenye busara hangalivuta sigara kamwe, hiyo ni kweli, iwapo ana mawaza.

²²³ Vema, nalidhania hiyo inaambatana na kanisa kabisa. Mwaona? Nawaza, je, Mungu ana chujio? Ndio.

²²⁴ Na kila kanisa lina chujio. Hiyo ni kweli. Wao huchuja wale wanaoingia, nao wanaingiza mauti nyingi pia.

²²⁵ Ungewezaje kamwe kuingiza dhehebu kupitia Chujio la Mungu? Ungewezaje kufanya hivyo? Ungewezaje kumwingiza mwanamke aliyekata nywele zake kupitia kwa Chujio hilo? Niambie. Ungewezaje kumwingiza mwanamke anayevalia suruali Mle, na huku “Ni chukizo kwake kuvaalia mavazi yampasayo mwanamume?” Mwaona, chujio la Mungu lingempata pale, halingemruhusu kuingia. (Bali makanisa yana chujio zao wenyewe.) Kwa hivyo nasema kuna chujio la mtu mwenyewe busara, hilo ni Neno la Mungu, nalo linafaa kwa ladha ya mtu mtakatifu. Hiyo ni kweli, mtu mtakatifu; sio mtu wa kanisa, bali ladha ya mtu mtakatifu. Kwa maana ni Neno la Mungu lililo safi na takatifu, lisiloghoshiwa! Ndilo hilo Chujio la mtu mwenye busara. Mfuasi wa kanisa, nakushauri utumie Hilo.

²²⁶ Kwa maana huingiza ulimwengu, na donge moja lake ni mauti. Donge moja huchachusha, chachu dogo huchachua donge nzima. “Mtu ye yote akiondoa Neno moja toka kwa Hiki, ama aongeze neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima.”

²²⁷ Katika Bustani ya Edeni, ni nini ilisababisha mauti, na huzuni hizi zote, kila kuvunjika moyo, kila mtoto mchanga anayekufa, kila kutatarika kwa koo, kila mlilo wa gari la kuchukulia wagojwa, kila hospitali, kila kaburi? Ilikuwa kwa sababu Hawa alitilia shaka Neno *moja* (si lote), hiyo ililipotosha tu. Sasa, Mungu alisema, “Mwanadamu,” pale, “ilimpasa kutii kila Neno la Mungu.” Naam, huo ni mwanzoni mwa Biblia.

²²⁸ Katikati ya Biblia, Yesu akaja, Naye akasema, “Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa *kila* neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Si sehemu Yake tu, kila moja.

²²⁹ Mwishoni mwa Biblia, Ufunuo 22, Yesu alitoa ushuhuda Mwenyewe. Ufunuo wa Biblia ni Yesu Kristo. Naye alisema, “Mtu ye yote atakayeondoa Neno *moja* Kwake, ama aongeze neno *moja* Kwake, sehemu yake itaondolewa kutoka Kitabu cha Uzima.

²³⁰ Sasa, pitia kwa Chujio *hilo* la mtu mwenye busara, utapata ladha ya mtu mtakatifu utokapo pale. Vema. Utapata ladha ya mtu mtakatifu.

231 Dada, wewe unayevalia hizo nguo, wazia hilo. Uta... Unasema, "Mimi ni mwadilifu kwa mume wangu." Mimi ni mwadilifu kwa rafiki yangu mwanamume. Mimi ni msichana mwadilifu. Lakini na yule mwenye dhambi aliyekuangalia? Atakapojibu kwa uzinzi, ni nani aliyetenda hivyo? Unaona, utakuwa mwenye hatia. Unaiona imeandikwa katika Neno, kwa hivyo... Waona? Lo, uwe mwanamke mwenye busara. Uwe mwenya busara...

232 Huenda ukasema, "Huenda ikawa..." Vema, vipi kama ingekuwa hivyo? Yeye alisema hivyo, na Neno moja haliwezi kutanguka. Waona?

233 Yule mtu mashuhuri aliniambia si muda mrefu uliopita, alinalika chumbani mwake, kasema, "Nitakuwekelea mikono, Ndugu Branham. Unaiharibu huduma yako, ukihubiri mambo kama hayo."

234 Nikasema, "Huduma yo yote ambayo Neno la Mungu litaharibu, inapaswa kuharibiwa." Waona?

235 Akasema, "Nitakuwekea mikono." Kasema, "Ulitembea kuombea wagonjwa."

236 Nikasema "Unaamini mambo hayo, ndugu?"

Akasema, "La. Lakini si wajibu wetu."

Nikasema, "Ni wajibu nani basi?" Unaona?

"Vema," akasema, "huo ni wajibu wa mchungaji."

237 Nikasema, "Watazame washiriki." A-haa. Hiyo ni kweli? Waona?

238 Kila mwaka napita nikuhubiri mambo haya, nami nawaza, "Hakika wamepokea," mwaka ujao narudi, wameongezeka zaidi. Waona? Hiyo ni kweli. Inaonyesha ya kwamba "Waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache!"

239 Uongozi ni Roho Mtakatifu, rafiki. Unakuongoza na kukutia kwenye Kweli yote, atakapokuja Roho Mtakatifu. Sasa wazia hayo. Chukua Chujio la mtu mwenye busara, hilo ni Biblia. Si kanuni zako za imani, si kanisa lako; utapotea. Chukua Chujio la mtu mwenye busara.

240 Hapo ndipo huyo kijana hakuwaza. Yeye alichukua chujio la kanisa. Akawa mtu anayependwa na watu wote, mtu mkuu, "Lakini kule kuzimu aliyainua macho yake, akiwa katika mateso.

241 Basi sasa chukua Chujio la mtu mwenye busara, Yesu Kristo, aliye Neno, nawe utatamani ladha ya mtu mtakatifu, kwa sababu itaridhisha hayo. Kama una Roho Mtakatifu ndani yako, Hili huridhisha.

242 Kama Roho Mtakatifu hayumo, unasema, "Lo, vema, sifikiri hilo lina tofauti yo yote." Tazama uliyotenda papo hapo! Jambo lile lile alilotenda Hawa. Umerudi mahali pale pale.

243 Basi na tuendeleo mbele zaidi. Sasa hebu tuchukue... tumwache huyo mtu hapa, ambaye hakutumia Chujio la mtu mwenye busara. Yeye alikataa kukubali uongozi wa Yesu Kristo na Uzima wa Milele.

244 Hebu sasa tuchukue kijana mwingine mfanyi biashara, mtawala, aliyekuwa na nafasi ile ile huyu mtu aliyokuwa nayo. Na kuukubali, yeye aliukubali uongozi wa Kristo. Naam, mna wawili wao katika Biblia ambao tutazungumza habari zao. Huyo tumeona ya kwamba aliukataa, basi na tumchukue mtu huyu: kijana mwingine tajiri mfanyi biashara, na mtawala. Naye aliukubali huo Uongozi.

245 Maandiko yanatuambia kuhusu huyu mtu, iwapo mnataka kuyaandika, Waebrania 11:21 hata 29:

...Musa, kwa imani, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao:

Akaona ni afadhali kupata mateso ya Mungu. . .

Akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri. . .

246 Mwaona, yeye alikubali Uzima wa Milele. Musa aliona kuwa ku—ku—kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina zote za ulimwengu. Musa aliona hayo ndiyo makuu sana. Basi, huyu tajiri hakuona hivyo.

247 Naye Musa alikuwa kijana tajiri na mtawala, atakayekuwa Farao. Yeye alikuwa mwana wa Farao, na mrithi wa kiti cha enzi. Naye akatazamia yasiyowezekana, kundi la wakanyaga matope, kundi la watumwa. Bali kwa imani akaona ahadi ya Mungu, kupitia kwa Neno, “Ya kwamba watu wake watakuwa wageni katika nchi ya kigeni kwa miaka mia nne, bali wangetolewa humo kwa mkono wenye nguvu.” Naye aliona Huo (haleluya) kuwa utajiri mkuu kuliko hazina zote za Misri, kwa maana alitoka Misri asijue alikokuwa akienda. Yeye aliongozwa na Kristo. Akatoka!

248 Mguu wake ulikuwa kwenye kiti cha enzi, naye angalikuwa halifa wa Farao Misri. Bali alihesabu kushutumiwa Kwake Kristo. Kushutumiwa! Kuitwa mtu wa “kipekee,” kuitwa “Mshupavu wa dini,” kuchukua mahali pake pamoja na wakanyaga matope na washupavu wa dini; kwa maana yeye aliona hiyo saa, hilo Andiko lililoahidiwa likitimizwa, ilikuwa basi imefikia.

249 Lo, kanisa basi, amkeni! Hamwezi kuona jambo lile lile usiku wa leo? Wakati ulioahidiwa umetufikia. Hesabuni kushutumiwa Kwake Yesu Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko ushirika wa cho chote, kiwe baba wala mama, kanisa, cho chote kile. Fuateni uongozi wa Roho!

250 Hebu tumfuatilie Kristo kidogo...huyu Musa kwa muda kidogo. Hapo, nilifanya hivyo. Hebu na tuyaangalie maisha yake.

Jambo la kwanza, alipokubali kuchukua kushutumiwa kwa Kristo na kuacha elimu yake, akaacha hekima yake yote. . . Yeye alikuwa amefundishwa kwa hekima yote ya Wamisri. Kupendwa kwake kwote na watu wote, kiti chake cha enzi, fimbo yake ya ufalme, ufalme wake, taji yake, kila alichokuwa nacho, alikikataa!

²⁵¹ Na mtu huyu mwingine aliyapenda, na akamkataa Kristo; na huyu mtu akakataa hayo, na kumkubali Kristo. Na upesi nini kilichotendeka? Ilimbidi kujitenga.

²⁵² Haleluiya! neno hilo, maana yake ni “Mungu wetu atukuzwe!” Ni vibaya sana kwamba tunalisahau.

²⁵³ Yeye alikataa viti vya enzi na kupendwa na watu wote. Yeye angaliwapata wasichana kwa. . . wake kwa mamia, naye angalipata fimbo za ufalme chini. . . Misri iliutawala ulimwengu! Ulimwengu mzima ulikuwa chini ya miguu yake, naye alikuwa mrithi wa kila sehemu yake. Bali kwa kuchunguza Maandiko na kuona siku aliyokuwa akiishi, na akajua ya kwamba Kitu fulani ndani yake, hiyo Mbegu ya Mungu iliyochaguliwa tangu awali ikaanza kufanya kazi.

²⁵⁴ Sijali ungependwaje na watu wote, ama ungekuwa *hivi* mara ngapi, ungekuwa mzee wa mkoa, ungekuwa mchungaji, ungekuwa *hiki*, *kile* au *kinginecho*, bali ikiwa hilo Neno la Uzima wa Milele kwa Neno la Mungu limekusudiwa ndani yako, na ukaona jambo hili limefika, itaanza kutenda kazi, kunjongea hivyo. Itaanza kutoka! Utaanza kulipata!

²⁵⁵ Naye akakataa kuitwa mwana wa binti Farao, kwa maana alihesabu kushutumiwa Kwake Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri ama ulimwengu. Yeye alihesabu huo. Tazama alichotenda, aliufuata. Akainuka, upesi akafukuzwa kwa watu wake, watu ambao wakati mmoja walimpenda.

²⁵⁶ Huenda ikakugharimu yote uliyo nayo. Huenda ikakugharimu nyumba yako, huenda ikakugharimu rafiki zako, huenda ikakugharimu karamu zako mamboleo, huenda ikakugharimu mahali pako kwenye kwaya. Huenda ikawa. Sijui itakugharimu nini, bali itakugharimu cho chote ambacho ni cha kilimwengu ama kinachohusiana na ulimwengu. Huna budi kujitenga na kila kitu ambacho ni cha ulimwengu. Huna budi kufanya hivyo.

²⁵⁷ Musa aliweka kila kitu kando na akaenda jangwani akiwa na kijiti mkononi mwake. Amina! Siku baada ya siku zikapita. Na si unashangaa iwapo alifanya kosa? La.

²⁵⁸ Mara nyingi watu huanza safari, nao wanasema, “Lo, nitafaulu. Mungu atukuzwe, naiona!” Na hebu mtu fulani akuchekelee na kukufanyia mzaha, “Huenda ikawa nalikosea.”

²⁵⁹ Yeye akasema, “Wale wasioweza kustahimili kurudiwa ni wana haramu wala si wana wa Mungu.” Mwaona, wao

waliwashwa-washwa tu. Mwaona, ile mbegu niliyonena habari zake muda mfupi uliopita, nafsi hiyo haikuweko kwanza. Ilikuwa na upako wa Roho, naye akatenda mambo mbali mbali. Lo, wewe na hao. . . Na wakati roho yako ina upako, unaweza. Ni Roho Mtakatifu halisi na wa kweli, hata hivyo ungeweza tu kuwa ibilisi.

²⁶⁰ “Lo,” unasema, “Ndugu Branham!”

²⁶¹ Manabii wa uongo! Biblia ilisema, “Katika siku za mwisho kutakuweko manabii wa uongo.” Yesu alisema, “Watatokea makristo wa uongo.” Si “ma-Yesu wa uongo,” sasa, Namna anayeweza kuvumilia hayo; bali “makristo wa uongo.” *Kristo* maana yake ni “walio na upako.” Walio na upako na ni wa mafuta wa uongo; wao wana upako, bali chanzo chao ni uongo, nao wanatenda ishara nyingi na maajabu, wananena kwa lugha, wakacheza kwa Roho, wanahubiri Injili.

²⁶² Yuda Iskariote alifanya hayo! Simeoni. . . au la, samahani. . . Kaiyafa alitabiri! Balaamu, yule mnafiki! Bila shaka, akafanya ishara zote, kila kitu, matendo yote ya kidini.

²⁶³ Lakini, mwaona, ukipanda punje ya gugu na punje ya ngano katika tuta ile ile na kuzimwagilia maji na kuzinyunyizia, zote mbili zitafurahi. Zote mbili zitachipuka kwayo, maji yale yale. “Jua huwaangazia wenye haki na wasio haki na mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki, bali kwa matunda yao mtawatambua.” Unawezaje kutoambatana na Neno? Amina. Mnaona ninayomaanisha? Maji huwamwagikia wenye haki na wasio haki, kuwanyunyizia.

²⁶⁴ Yesu alisema, “Watakuja kwangu siku ile, wakisema, ‘Bwana! Bwana! Sikutoa pepo? Sikutabiri? Sikufanya mambo makuu katika Jina Lako?’” Yeye atasema, “Ninyi mtendao maovu, ondokeni Kwangu, hata siwajui. Enendeni kwenye kuzimu kwa milele alikowekewa tayari Ibilisi na malaika zake.” Mnaona? Ni Neno jinsi gani! Wa uongo. Huabudu bure, hujitahidi bure. Mbona mnafanya hivyo na huku haiwapasi kufanya hivyo? Mbona mchukue mwigizo na humu mbingu zimejaa yaliyo halisi? Mwaona? Haiwapasi kufanya hivyo.

²⁶⁵ Sasa tunamwona Musa aliyekuwa na upako, hamna kingalimrudisha nyuma. Ndugu zake mwenyewe walimkataa, hilo halikumkomesha. Yeye aliendelea mbele hata jangwani. Na siku moja kule, kakutana na Mungu uso kwa uso, pamoja na Nguzo ya Moto iliyoning’inia kwenye kijiti. Kasema, “Musa, toa viatu vyako, mahali hapa unaposimama ni patakatifu. Kwa maana nimesikia vilio vya watu Wangu, pia nimesikia kuugua kwao, nami nimekumbuka ahadi Yangu ya Neno. Nami ninashuka, nitakutuma kule ukawatoe.” Bila shaka. Yeye alikutana na Mungu uso kwa uso, akazungumza naye. Yeye aliagizwa na Mungu.

266 Mungu akarudi moja kwa moja. Nguzo hiyo hiyo ya Moto, na kumthibitisha huyo nabii aliyesimama mlimani; kuthibitisha ilikuwa hivyo alipoitwaa mikono yake na kufanya miujiza ya kila namna na kadhalika. Lo, walikuwa na waigaji. Lo, hakika. Kulikuweko Yambre na Yane waliosimama papo hapo na kutenda jambo lile lile walilotenda. Bali nani alikuwa wa kwanza? Mwaona? Ilianzia wapi? Ilitoka kwa Neno? Ilikuwa wakati unaofaa?

267 Je, mnajua jambo lilo hilo limeahidiwa tena katika siku za mwisho? “Kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Musa, vivyo hivyo watu hawa, watu waliopotoka akili zao na waliokataliwa kwa mambo ya Kweli.” Mwaona, katika siku za mwisho. Na kufanya jambo lile lile, (kuiga kila kitu), kwenye mlolongo ule ule, “Nguruwe akirudi kugaa-gaa, na mbwa akiyarudia matapiko yake.”

268 Nanyi Wapentekoste mliotoka katika hayo madhehebu miaka kadha iliyopita na kuyalaani, baba na mama zenu, nanyi mkageuka moja kwa moja na kufanya jambo lile lile walilofanya, na sasa ni kugaa-gaa kule na matapiko yale yale. Mwaona? Iwapo ilifanya Kanisa litapike hayo katika nyakati za mwanzoni za Kipentekoste, italifanya litapike tena leo. Mwaona? Halina budi kuwa, ingawaje, ni kapi. Halina budi kuja. Kishada hakiwezi kuwa peke yake; kapi halina budi kuja, mwaona, mbebaji. Sasa tunaishi katika siku za *mwisho*, tazama mambo yaliyoahidiwa kwa wakati huu.

269 Mtazame huyu Musa akithibitishwa. Jua! Alipopanda kule, baadhi ya ndugu zake walimchukia, walitaka kufanya dhehebu. Wao walisema, “Unatenda kama kwamba ndiwe mtu mtakatifu miongoni mwetu.” “Makutano yote ni watakatifu,” kasema Kora, Dathani.” Na tumchague mtu na kutenda jambo fulani.”

270 Musa yeye. . . nilimsikitikia. Akashuka akaenda na kusema, “Bwana. . .” Kaanguka mbele ya madhabahu na kusema, “Bwana. . .”

271 Mungu akasema, “Jitenge nao. Nimechoka nao.” Akafungua tu nchi nayo ikawameza. Mwaona, yeye alijua agizo lake.

272 Mungu hashugulikii madhehebu, Yeye hashugulikii Makundi. Yeye hushughulikia watu binafsi. Hiyo ni kweli. Kila mara. Si katika makundi; watu binafsi, mtu mmoja. Katika siku za mwisho, Yeye alisema, “Nasimama mlangoni, nabisha; na iwapo mtu ye yote. . .” (si “kundi lo lote”) “. . .mtu ye yote akisikia Sauti Yangu, nita. . .na kunisikia Mimi, nitaingia kwake na kula.” Mnaona, “Kama mtu ye yote anaweza kusikia.”

273 Hii—hii maikrofoni inawezaje kutoa sauti yangu kule nje kama haikutengenezwa hivyo? Ningeupigia kelele ule ubao, kwa nguvu zangu zote, na hautafanya cho chote. Kwa sababu hii imekusudiwa, ikafanywa, ikaumbwa, kuwa maikrofoni. Na iwapo Neno la Mungu limo ndani yako kwa kukusudiwa

awali na Mungu, ndani yako, “Kondoo Zangu huisikia Sauti Yangu. Wanajua sauti Yangu. Mgeni hawatamfuata.” Mwaona, Inapaswa kuwa hivyo kwanza. “Wote alionipa Baba, watakuja.” Kila mmoja wao, mwaona.

²⁷⁴ Basi, anaendelea, hata mwisho wa uhai wake hapa. Yeye alipita tu . . . Tazama alipofikia mwisho wake.

²⁷⁵ Na tunafunga sasa kwa maana inachelewa, saa nne kasoro dakika ishirini na tano. Tazama. Naam, kule nyumbani hiyo ni mapema. Yapata saa nane ama saa tisa tunaanza kusema, “Aisee, inaanza kuchelewa kidogo.” Mnaona? Mwaona? Lakini sasa, nimehubiri siku nyingi usiku, usiku kucha.

²⁷⁶ Paulo alihubiri Injili ii hii katika siku zake, na kijana fulani akaanguka u—ukutani akafa. Naye Paulo, akiwa na upako ule ule na Injili ile ile, akauweka mwili wake juu ya wake, akaishi tena. Walikuwa na hamu. Kanisa lilikuwa likiundwa. Jambo fulani lilikuwa likitendeka. Tazama kilichotendeka hapa.

²⁷⁷ Musa, aliposhuka chini . . .

²⁷⁸ Huyu tajiri, aliposhuka akaja, yule kijana mtawala tuliyenena habari zake, amejaa dini, na alikuwa mshiriki wa kanisa na kadhalika, mtu mzuri, aliyelimika, mfanyi biashara mzuri, na kila kitu, alipofikia mwisho wake, akaanza kupaza sauti, “Hamna mahali pa kukanyanga!” Uongozi wake uko wapi? Alikuwa ameongozwa na kanisa lake, ambalo ni maiti. Alikuwa ameongozwa na ulimwengu ulio maiti, na hapakuwepo cho chote cha kukanyagia ila kile ulimwengu ulikuwa umeitayarishia: kuzimu.

²⁷⁹ Bali hapa yuaja Musa, mtumishi mwaminifu aliyehesabu kushutumiwa kwa Kristo kuwa ni hazina kuu kuliko utajiri wote wa Misri. Akafikilia kikomo chake, mzee, umri wa miaka mia moja na ishirini. Akapanda mlimani, naye alijua ya kwamba mauti yalikuwa mbele yake, naye akatazama kuelekea nchi ya ahadi. Naye akatazama; pale amelala karibu naye, alikuwa Kiongozi wake, yule Mwamba. Akaukanyanga ule Mwamba, nao Malaika wa Mungu wakambeba wakampeleka kwenye Utukufu—Utukufu wa Mungu katika kifua cha Mungu. Kwa nni? Miaka mia nane baadaye, alikuwa bado anaongozwa na Kiongozi wake.

²⁸⁰ Tunamwona kule kwenye Mlima wa Kugeuziwa, amesimama pale na Eliya, akizungumza na Yesu kabla hajaenda msalabani. Miaka mia nane baada ya kifo chake, ambaye yeye . . . Yule, yeye alihesabu kushutumiwa kwa huduma Yake kuwa ni hazina kuu kuliko kupendwa kote na watu wote wa ulimwenguni na fedha zote za ulimwenguni, Kiongozi wake alikuwa bado yu anamwongoza. Lo, jamani! Yeye aliongozwa! Kiongozi Wake, aliongoza kupitia mautini, vivuli vya mauti. Yeye aliongozwa hata kaburini. Mamia ya miaka baadaye, ndiye huyo amesimama pale tena, kwa sababu katika ujana wake, yeye aliisha kuchagua

uongozi wa Roho Mtakatifu. Jina lake litakuwa kuu wakati hakutakuweco Misri wala hazina tena. Piramidi zitakapokuwa mavumbi, na wakati Misri haitakuwa tena Misri, Musa atakuwa asiyekufa miongoni mwa watu maana alikubali uongozi wa Kristo badala ya kwenda jinsi kanisa lake lilienda.

²⁸¹ Kuna wengine waliotenda jambo lile lile. Mtazameni Henoko. Yeye akaenda pamoja na Mungu kwa miaka mia tano, ndiposa akashuhudiwa ya kwamba “Amempendeza Mungu.” Mungu akaithibitisha, akasema, “Hapana haja kwako kufa, panda tu juu uje Nyumbani alasiri ya leo.” Naye akapanda hata juu.

²⁸² Na Eliya. Baada ya kuwakemea sana wanawake waliofupisha nywele zao na kila kitu, kama alivyotenda katika siku zake, Mayezebeli wenye kujipaka rangi, baada ya kuchoshwa nayo, na—na alikuwa ametenda yote aliyoweza, na hao makuhani wote wakimfanyia mzaha, na kila kitu, yeye alishuka akaenda mtoni siku moja. Na ng’ambo ya pili ya huo mto mlikuwemo farasi waliofungiliwa kwenye kijiti mle, gari la moto na farasi wa moto. Mara yeye akalipanda, kisha akamtupia nabii atakayemfuata joho lake, akapanda kwenda Mbinguni. Yeye alikubali uongozi wa Uzima wa Milele, maana ilikuwa Kristo aliyekuwa katika Eliya. Lo! Naam, bwana!

²⁸³ Ilikuwa nini? “Nifuate!” Sasa huna budi kuchagua kiongozi wako. Hamna budi kumchagua, marafiki. Tazama kwenye kioo cha Mungu cha kutazamia, Biblia, na uono uliko usiku wa leo.

²⁸⁴ Hadithi dogo. Mtoto mchanga, wakati mmoja, aliishi mashambani. Hakuwa amepata kuona kioo, naye akaja mjini kumwona dada ya mamaye. Naye alikuwa na makao . . . na hayo makao mtindo wa kale yalikuwa na kioo mlangoni; sijui kama mnakumbuka hiyo au la. Bali huyu kijana, hakuwa amepata kuona kioo. Kwa hivyo yuacheza nyumbani, naye akatazama kwenye . . . “A-haa?” Akamtazama huyu kijana mdogo. Kisha akampungia mkono, naye huyo kijana mdogo akapunga mkono. Halafu akavuta sikio lake, naye huyo kijana mdogo akavuta sikio lake. Na kuendelea hivyo. Akazidi kusongea mbele, kukaribia, kisha akageuka na kusema, “Mama! Huyu ni mimi!” Huyu ni mimi.

²⁸⁵ Je, *wewe* unafanana na nini? *Wewe* unafuata nini? Tumefanyaje? Huna budi kuchagua *kiongozi* wako. Chagua leo. Unachagua Uzima au mauti. Chaguo lako litaamua kikomo chako cha milele, unachochagua. Kumbuka, Yesu alisema, “Unifuate.” Umealikwa usiku wa leo kufanya hivyo. Na kumfuata hata kwenye Uzima wa Milele huna budi kukubaliana na masharti Yake, hiyo ni kweli, Neno. Si juu ya kanuni za imani, si kulingana na maoni ya watu, si kulingana na yale mtu ye yote analiwazia, bali aliyosema Mungu kulihusu.

²⁸⁶ Unasema, “Vema, Ndugu Branham, namjua mwanamke mzuri vilivyo, yeye hufanya *hivi*. Namjua mwanamme fulani aliyepitia *haya*.”

²⁸⁷ Sijui waliyofanya. Neno la Mungu, Yeye alisema, “Neno la kila mtu liwe la uongo, na Langu Kweli.” Huna budi kutimiza masharti Yake, kuja kulingana na kanuni Zake, Neno. Hauwezi kuja kupitia kanuni za imani, hauwezi kuja kupitia dhehebu, hauwezi kulichanganya hivyo. Kuna jambo moja tu unaloweza kutenda: likubali kulingana na masharti Yake, ya kwamba wewe u tayari kujifia mwenyewe na mawazo yako yote, kisha umfuate Yeye. “Tupilia mbali mambo yote ya kilimwengu, kisha unifuata.”

²⁸⁸ Najua huo ni Ujumbe mgumu, unaoumiza, ndugu. Bali sikuja hapa na kuchagua u—ujumbe kwa watu ili kuwafanya waimbe, wapaze sauti; wapige ukelele. Nimekwisha kuwa katika mikutano ya makafiri ambako walitenda jambo lile lile. Ninayajali maisha yako. Mimi ni mtumishi wa Mungu ambaye hana budi kujibu mbele za Mungu hivi karibuni, na huduma ambayo Bwana amenipa imejithibitisha mara elfu kadha mbele zenu.

²⁸⁹ Kumbukeni, Yesu alisema, “Unifuata. Unifuata. Ondolea mbali uliyo nayo, ukanifuata.” Na hiyo ndiyo njia pekee ya kupata Uzima wa Milele. Hilo ndilo shauri pekee alilompa mtu huyu, ndilo shauri pekee Yeye alimpa huyu mfanyi biashara, ndilo shauri pekee ampalo mtu ye yote. Chaguo Lake, Yeye afanyapo maamuzi, ni makamilifu kila mara. Nasi hatuna budi kumfuata, ndiyo njia pekee ya kupata Uzima wa Milele. Kwa hivyo uongozi wa Mungu ni: fuata Neno lililothibitishwa la wakati huu na Roho Mtakatifu.

Na tuinamishe vichwa vyetu:

²⁹⁰ Nitawaulizeni swali, nami nawatakeni muwe waaminifu sana. Nataka dada anichezee huu, *Naweza Kumsikia Mwokozi Wangu Akiita*. Nataka mwaliko wa madhabahuni wa mtindo wa kale. Na ndugu, dada, tunapoona, hebu tazama tu yanayotendeka siku hizi. Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, hebu wazeni kwa muda mdogo, tazameni yale yanayotendeka.

²⁹¹ Mlisoma gazetini juma lililopita yale yule mtu kule Uingereza aliyosema? Ya kwamba “Kusulubiwa kwa Yesu Kristo kulikuwa tu kwa bandia, kulikuwa hila ya Pilato pamoja Naye.”

²⁹² Mliona yale mwanatheologia wa Kiamerika aliyosema? Alisema ya kwamba “Yesu alitiwa usingizini kwa tunguja.” Wengi wenu wanatheologia mnajua, kule nyuma katika Mwanzo ambapo inanena kuhusu tunguja. Itakutia usingizini kama kwamba u mfu, moyo wako haupigi ila kwa zamu muda wa siku mbili au tatu. “Na walipompa siki na nyongo,” wao walisema, “hiyo ilikuwa tunguja. Na wakamweka mle kaburini, naye

akalala mle siku tatu. Kisha, bila shaka, walipoenda kule, wakampata akitembea pale.” Ungewaza hilo! Wanatheologia, seminari, waona, kujifanya waamini. . . [Mahali patupu kwenye ukanda—Mh.] Vipi basi, yawezekanaje na huku Biblia hata inasema ya kwamba Yeye alikataa? Walipotia siki na nyongo kinywani Mwake.

²⁹³ Jambo lingine, ikiwa hiyo ni kweli, basi mbona hao wanafunzi “waliokuja wakamwiba,” mbona wakatoa maisha yao katika ufa imani kwa ajili Yake? Nao wakaanguka, wakajihesabu wenyewe wasiostahili hata kufa kama Yeye alivyokufa; wakapinduliwa juu chini na upande-upande msalabani na kadhalika. Na ikiwa wao walikuwa. . . walijua ya kwamba Yeye alikuwa mnafiki nao wenyewe wakiwa wanafiki, wangetoaje uhai wao kwa ajili Yake hivyo?

²⁹⁴ Lo, mwaona, ni siku hizi za kiakili tunamoishi. Elimu, ustaarabu, na mienendo ya siku hizi, yote ni ya Ibilisi. “Ustaarabu na wa Ibilisi?” Naam, bwana! Biblia ilisema ni wake. Ustaarabu huu una mauti. “Je, tutakuwa na ustaarabu kama huu katika ulimwengu ujao?” La, bwana! Tutakuwa na ustaarabu wa aina nyingine. Elimu, mambo haya yote, yote ni ya Ibilisi; sayansi inapotosha mambo ya kawaida, ikitengeneza kitu kingine.

²⁹⁵ Tazameni waliyowafanya ninyi sasa. Wakati vijana wanawake. . . *Reader's Digest* ilisema, wiki. . . miezi miwili iliyopita, naamini ndivyo ilikuwa. *Reader's Digest* ilisema ya kwamba “Vijana wanaume na wanawake huwa watu wa makamu, wanawake huungia ugumba kati ya umri wa miaka ishirini na ishirini na mitano.” Kizazi, kimoja zaidi, hawatakuwa kitu ila. . . Watakuwa wakionekana wa kuchukiza. Waona? Watakuwa viumbe wa namna gani, wadhaifu, goigoi. Tazama nafsi, tazama roho, tazama jinsi roho kanisani imekuwa, mbegu iliyochanganyishwa, limeolewa na ulimwengu. Jamani, ni majira ya namna gani! Kimbieni enyi watoto! Kimbieni! Kimbieni Msalabani! Njoooni Kwake Kristo, mwacheni awaongoze.

²⁹⁶ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, macho yetu yamefungwa, na sasa tafadhali inamisheni mioyo yenu pia. Mtafanya hivyo? Nataka kuwaulizeni, swali. Je, unajitazama mwenyewe, mbele za Mungu? Na je, unajisikia ya kwamba wewe huko ambako u—unapaswa kuwa katika majira haya? Kwa maana kunyakuliwa kunaweza kuja wakati wo wote. Waona, kutakuja.

²⁹⁷ Kungekuweko, kama—kama tamshi nililofanya muda mfupi uliopita ni kweli, kutakuweko tu yapata watu mia tano katika kunyakuliwa, wanaoishi, watakaobadilishwa. Naam, tukijumlisha Ukristo wote, Katoliki na kadhalika, kuna watu milioni mia tano, waona, wanaodai Ukristo. Na mmoja toka kila milioni watakuwa watu mia tano. Kuna watu kama hao wanaopotea kila siku, kote ulimwenguni, ambao hata hatuwezi

kuwatolea hesabu. Mnaona, kutakuja, na hata hamtajua habari zake. Watu wataendelea kuhubiri, wakisema...Mwaona, na kutakuwa kumepita.

²⁹⁸ Kama Yesu alivyosema. Wao walisema, hao wanafunzi walisema, “Mbona waandishi, husema, ‘Eliya hana budi kuja kwanza?’”

²⁹⁹ Yeye akasema, “Amekwisha kuja, wasimtambue, bali walimtendea yale waliyosema wangemtenda.”

³⁰⁰ Unajua ya kwamba hupatani na Mungu, na ungetaka kukumbukwa...kwa Mungu, ya kwamba Mungu angeipatanisha moyo yako na Mungu. Je, waweza kwa unyenyekevu sasa, katika wakati huu mtulivu sana, kuinua mikono yako? Sijali wewe u nani, ungefanya hivyo? Useme, “Nitamwinulia Mungu mikono Yangu.” Mungu akubariki. Mungu akubariki.

³⁰¹ Je, unatazama kwenye Kioo? Nakuuliza katika Jina la Kristo, Je, unaangalia Kioo cha Mungu? [Ndugu fulani ananena katika lugha. Ndugu mwingine anatoa tafsiri—Mh.] Amina.

³⁰² Nataka kuuliza neno moja. Je, ni wangapi walio humu ndani ambao ni Wapentekoste? Inueni mikono yenu, mlio Wapentekoste. Karibu kila mmoja wenu. Basi, wangapi ndani humu wanadai kuwa Wakristo? Inueni mikono yenu, po pote mlipo, mnaodai kuwa Wakristo. Je, mnajua Biblia ilinena juu ya haya, ya kwamba haya yatatendeka.

³⁰³ Hata haya yalitendeka katika Agano la Kale walipokuwa wakishangaa wafanye nini, jinsi wangaliepuka kuzingirwa ambako kulikuwa kwaja. Roho alimshukia mtu fulani naye akatabiri na kuwaambia mahali ambapo wangemkabili adui, na jinsi, ambavyo wangemshinda huyo adui. Hiyo ilikuwa Agano la Kale, sawa na Agano Jipya.

³⁰⁴ Basi, mtu fulani huenda akasema, “Mtu huyo, lo, hivyo sivyo ilivyokuwa.” Lakini vipi ikiwa ndivyo ilivyo. Unasema, “Lo, nimesikia hayo hapo awali.” Lakini vipi kama *hili* liko hivyo? Mwaona, hiyo inathibitisha ya kwamba humu ndani mna watu wengi wanaohitaji geugo la moyo, iwapo huyo ni Roho Mtakatifu anayenena. Mna mambo yanayohitajika kutendwa, kwa hivyo yako kwako.

Nitwae hivi nilivyo,
Umemwaga damu yako,
Nawe ulivyo niita... (hivyo ndivyo alivyokuita
basi)

Bwana Yesu naja... (Nitaondoa huyo moyo
mkaidi, na kuweka moyo wa nyama
ndani yake ambao ungejitolea Kwangu.”
Waona)...naja!

Hivi nilivyo; si langu
 Kujiosha... (Je, utajichagulia usiku wa leo?
 Unaweza kufanya lo lote utakalo)...
 moyo,... (Unasema, "Nimesikia hayo hapo
 awali." Bali huu waweza kuwa wakati wa
mwisho utakaosikia)
 Nisamehe dhambi zangu,
 (Ile mialiko ya kikale ya madhabahuni,
 haitumiki tena siku hizi, bali Mungu yu
 angali anatenda kazi kwake. Je, hamwezi
 kuusikia ukitenda kazi ndani yenu,
 kanisa?)... naja!

³⁰⁵ [Ndugu Branham anaanza kuguguniza *Nitwae Hivi Nilivyo*—Mh.] Jamani, wazia, siku hizi, miyo inakuwa ya kijiwe, imejazwa kilimwengu, kutojali, wafuasi wa kanisa, wenye uvuguvugu, kama yule kijana tajiri na mtawala; na hawajui ya kwamba Roho Mtakatifu aliye mkuu yuasimama akibisha mlango katika wakati huu wa Laodikia. "Yeye atakayeisikia Sauti Yangu (Neno), atakayefungua moyo wake, nitaingia ndani yake na kula pamoja naye."

³⁰⁶ Naye Roho akinena kupitia kwa ndugu huyu dakika chache zilizopita, alisema, "Nitaondoa huyo moyo wa jiwe ndani yenu, na kuwapa moyo wa nyama, mwororo kwa Mungu." Tazama jinsi umekuwa sasa, wa kiakili tu, wa mahangaiko tu. Waona? Si moyo mwororo uliojaa upendo na utamu kwa Kristo.

³⁰⁷ [Ndugu Branham anaanza kugugumiza ile pambio—Mh.] Je, hamtaki moyo wa namna hiyo? Je, utamkabilije Kristo ukiwa na mawazo tu ya kiakili juu Yake? Huna budi kukubali Uzima wa Milele.

...umemwaga damu... (matayarisho
 yalifanywa kwa Damu)
 Nawe ulivyo niita... (Je, Yeye alifanyaje?)
 Akamwaga Damu Yake; na sasa akuita njoo...
 ulivyoniiita,
 Bwana Yesu naje! Naja!

³⁰⁸ Hebu, kila Mkristo, inueni mikono yenu tu kwa utulivu na kuomba.

³⁰⁹ Ee Mungu, tafadhali, Mungu, ishike siku hii tunamoishi. Lo, ni vigumu sana, Baba. Shetani ametenda mengi sana kwa hawa watu Mioyo yao imekuwa ya jiwe. Roho Wako ananena wazi wazi; Neno Lako linasonga mbele, linathibitishwa; bali ule mtindo wa kale wa ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili, wao... umekuwa wa mawazo ya kidhehebu, na kiakili, muziki mwingi, kupiga kelele kwingi, na kutenda kwingi yasiyofaa. Lakini, hakika, huyo moyo wa nyama, Roho huyo, huo Uzima wa Milele, bila shaka umekuwa wa kigeni kwa kanisa.

310 Mungu, inavunja moyo wangu, na mimi mwe-mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yako. Inanifanya kujisikia vibaya sana, Baba, kuona hilo kanisa ulilolifia, kanisa unalojaribu kukomboa. Nawaza kuhusu lile ono ambalo umenionyesha kuhusu hilo kanisa la Marekani na ya nchi zingine. Jinsi lilivyoonekana la kuchukiza, wenda uchi wacheza rumba. Bali mahali pengine pale nikaona lingine likija, lililobarikiwa.

311 Naomba, Baba, ya kwamba kama ye yote wa wale hapa usiku wa leo waliokusudiwa Uzima, ama wangetaka kuukubali, ya kwamba huu utakuwa wakati watakaofanya hivyo. Tujalie Bwana. Vunja moyo wa jiwe sasa, ule moyo wa kale wa kidunia. Na iwapo wanataka amani, wanataka jambo linalotosheleza, jambo linalotoa matumaini, na hao wakubali uongozi wa Yesu Kristo usiku wa leo kuwaongoza hata kwa A—Amani ipitayo akili zote, Furaha isiyoneneka, yenye utukufu, ama hata kitu ambacho mauti yenyewe hayawezi kudhuru. Tujalie, Baba.

312 Sasa, huku mikono yetu imeinuliwa, nashangaa kama. . . Wangapi humu chumbani sasa wangesema, “Mimi nitasimama.” Basi, sijali ni nani anayeketi kando yako; ni Mungu anayenena nawe. Na hakika unataka kuwa Mkristo halisi, waona. Cho chote ambacho kita. . . Na chini ya hiyo ni muigizo; lo, heri niendeleo tu na kuwa katika ulimwengu. Naamini ungefanya hivyo, pia.

313 Sasa, jichunguze tu kwa Neno, kwa Ujumbe. Chunguza jinsi Mkristo halisi anavyopaswa kuwa: asiye wa kawaida, mwenye upendo, si moja wa huu Ukristo mamboleo. Naam, ni mdhaifu, unaopindika, umekufa nusu, umeoza, mchanganyiko. Waona, si Ukristo halisi; wanaishi maisha yo yote, na kuwa wafuasi wa kanisa. Je, hutaki huo ushirika mtamu pamoja na Kristo, Roho Mtakatifu, ili uwe. . . roho yako ifanane na Neno? Songa mbele hata kwa Kristo. Kama unataka hivyo, na ungetaka Mungu kuona msimamo wako usiku wa leo papa hapa kwa hili kundi la watu, iwapo utafanya hivyo tu.

314 Unasema, “Je, hilo litamaanisha kitu, Ndugu Branham?”

315 Naam. Bila shaka, itamaanisha. “Kama ukinionea haya Mimi mbele ya watu, nami nitakuonea haya mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu. Bali kila mtu atakayenikiri Mimi na kunitetea katika nchi hii, nitamtetea katika nchi hiyo. Nitamkiri mbele za Baba Yangu.”

316 Basi, si hoja u nani, mwanamke, mwanamume, mvulana ama msichana, ye yote uliye. Mkristo si Mkristo, muhudumu, shemasi, ye yote uliye, iwapo utaamini tu kwa moyo wako wote, kwa muda mdogo tu, na kufanya haya usiku wa leo kumfanya Mungu ajue ya kwamba u mwaminifu. “Mungu. . .”

317 “Sasa tazama, mimi ni Mpetekoste,” unasema. “Mimi ni *hiki*,” ama cho chote ulicho. “Ninakiri kucheza katika Roho.

Lakini, Ndugu Branham, nilidhani mradi tu tulikuwa hivyo, tumeupata.” Hamna.

318 Kama mnaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu, sikizeni basi Maneno yangu. Mwaona? Huo ndio udanganyifu wa siku hizi. Biblia haikusema zingefanana sana hata ingewadanganya walio Wateule kama yamkini? Walio *Wateule*, “hata nafsi.”

319 Bali kama ulicheza katika Roho, na ungali una mambo ya duniani, mna walakin. Kama unanena kwa lugha; Paulo alisema, “Naweza kunena kwa lugha za wanadamu na za malaika, na hata sijaokolewa.” A-haa, aina zote mbili, waona. “Naweza kufurahi sana, naweza kuwa na imani, naweza kuhubiri Injili, naweza kutoa mali yangu yote nikawalishe maskini, naweza kupeleka Neno kwa umishenari kote ulimwenguni, na bado si kitu mimi.” Mnaona? Ni kile kilicho Ndani cha upande wa ndani, ndugu. Hiyo. . . Roho yako huondoka unapokufa, inaruka, bali nafsi yako inaendelea kuishi. Waona?

320 Sasa, jitazame mwenyewe. Kwa kweli, wewe ni Mkristo halisi wa Biblia, aliyejaa upendo wa Mungu? Kumbuka, Biblia ilisema, katika siku za mwisho wakati huu utakapofika, Yeye alisema, “Malaika wa kutia alama alipitia makanisani, akapitia mijini, na kutia muhuri wale tu waliougua na kulia kwa sababu ya machukizo yaliyofanyika mjini.” Hilo ni kweli? Ezekieli 9, tunajua hiyo ni Kweli. Yule malaika wa kutia alama akatoka akaenda na kutia Alama vichwani mwao, katika vipaji vya nyuso zao, akawatia muhuri, “Hao waliougua na kulia.”

321 Kisha wakaja malaika wa kuangamiza kutoka pande nne za nchi, ambao wanakuja hivi sasa, tunaona vikija, vita vikali moja kwa moja ambavyo vitaangamiza dunia nzima. Hamna kitu wasingaligusa ila hao waliokuwa na ile Alama.

322 Sasa jichunguze. . . Je, moyo wako unahusika juu ya wenye dhambi, na jinsi kanisa na watu wanafanya, hata waweza kuugua na kulia juu yake mchana na usiku? Kama sivyo, nashangaa. Hayo ni Maandiko.

323 Je, waweza tu kusimama na kusema, Mungu mpendwa, mimi sisimami kwa sababu Ndugu Branham alisema hivyo, bali nalisikia Neno lake likisema hivyo, nami nitafanya hivi. Kwako, Bwana, nasimama. Mimi ni mhitaji, Bwana. Je, utanipa mahitaji yangu hapa usiku wa leo mahali hapa? Nasimama.” Mungu akubariki Mungu akubariki. “Mimi ni mhitaji, nakutaka unirehemu.” Mungu awabariki. “Nataka kuwa Mkristo ambaye. . .”

324 Sasa, kumbuka, huyo mtu anayesimama karibu nawe ni kama wewe. Nakutaka unyoshe mkono wako ukaushike wake, ukasema, “Ndugu, dada, niombee sasa. Nakutaka uniombee. Ni—ni. . .” Sema hayo tu kwa unyenyekevu wa Kikristo, “Niombee. Nita. . . Na—na—nataka kupatana na Mungu.

Niombee mimi, nitaomba ya kwamba Mungu atakupa nafasi hiyo.”

³²⁵ Na—najua ya kwamba sisi tuna...Hatuwezi kukaa hapa muda mrefu zaidi; mnaona hivyo. Tuko—tuko katika wakati wa mwisho. Wote wanaoamini hayo, semeni, “Amina.” [Makutano wanasema, “Amina!”—Mh.] Tuna...Hamna kilichobakia. Kila kitu kimekwisha. Makanisa yanaelekea kwenye baraza la Ekumenia. Ulimwengu, una...

³²⁶ Tazama hapa! Je, mnajua Bwana asemayo kuhusu Los Angeles na mahali hapa pengine? “Umekwisha!” Mnakumbuka niliyowaambieni, yapata miaka miwili iliyopita, jinsi hilo tetemeko la nchi lingekuja Canada, kule Alaska? Nawaambia pia ya kwamba “Hollywood na Los Angeles zinadidimia kuingia baharini. California, umeangamia! Si California, tu, bali wewe, ulimwengu, umeangamia! Kanisa, isipokuwa mpatane na Mungu, mmeangamia!” ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI!

³²⁷ Je, mmenisikia nikitumia Jina hilo isipokuwa itimie? Nawaulizeni! Mmenijua kwa muda wa miaka ishirini. Je, nimewaambia neno lo lote katika Jina la Bwana ila lile lililotimia? Ikiwa kila kitu nilichowaambieni kingetendeka, kilitendeka, semeni “Amina.” [Makutano yanasema, “Amina!—Mh.] Nawaambieni, huu ndio wakati, yawapasa kujitayarisha, sisi sote.

Basi, na kila mtu amwombee mwingine:

³²⁸ Mungu mpendwa, tunaposimama hapa usiku wa leo, watu wanaokufa, nyuso zetu zimeelekezwa ardhini, mavumbini. Sisi...Umetupa mahubiri haya yanayokata, Bwana. Tunaona mifano ya watu wawili. Mmoja wao, akiwa mtu wa kidini, alienda kanisani bali akakataa uongozi hata Uzima wa Milele. Na yule mwingine alikataa sifa za ulimwengu na *kugeukia* Uzima wa Milele. Nasi tunaona hall za hao wawili usiku wa leo, kulingana na Biblia: yule tajiri katika mateso, na Musa Utukufuni.

³²⁹ Baba tunataka kuwa kama Musa. Tunataka kuongozwa na Mwanao Mtakatifu, Yesu Kristo, hata kwa Uzima wa Milele. Utupe huo mioyoni mwetu usiku wa leo, Bwana. Ipasue ile mioyo ya kale ya jiwe; weka ndani yetu moyo mpya, moyo wa nyama, moyo anaoweza kuuzungumzia na kuushughulikia, nasi hatutakuwa wenye kiburi ama wasiojali. Na Roho Mtakatifu asiondoke kamwe, Bwana. Na aje na kuwaagiza watu hawa. Nena nao; rarua nia zao za jiwe, na uweke ndani yao nia ya Mungu. Okoa kila mmoja, Baba. Tupe upendo Wako. Tufikishe mahali, Bwana, ambapo tutaondokea se—sehemu yote ya kuchangamka, tufikie sehemu hasa ya kujisikia sehemu ya kujisikia kwa moyo, kilindi cha Roho, utajiri wa Mungu, Ufalme wa Roho mioyoni mwetu. Tujalie, Ewe Kiongozi Mkuu,

Roho Mtakatifu aliye mkuu, kabla hujaruka angani pamoja na Kanisa Lako.

³³⁰ Ee Mungu, hebu niondoke, Bwana. Usiniache nyuma, Yesu. Hebu niende pamoja Nawe, Baba. Sitaki kukaa hapa duniani humu kuona haya mateso yanayokuja. Sitaki kukaa humu katika wenda wazimu huu. Sitaki kuwa humu wakati mambo ya kutisha . . . watu wakirukwa na akili zao. Tunawaona watu wakijaribu kutenda kama wanyama na kuonekana kama wanyama; na wanawake wakijaribu kuonekana kama wanyama, wakijipaka rangi nyusoni mwao. Tukijua ya kwamba mambo haya yametabiriwa kutendeka, kwamba jambo hilo litatendeka, watakuwa wazimu sana hata nzige watainuka wakiwa na nywele kama za wanawake kuwatesa wanawake; na meno kama simba, na mambo ambayo Wewe umesema, na akili za watu zitawaruka kabisa. Tunaona yakianza kutendeka sasa hivi, Bwana. Tusaidie! Turudishie akili timamu ya Kristo Yesu Bwana, wetu.

³³¹ Ee Kiongozi Mkuu wa Uzima wa Milele, tunakubali ahadi Yako usiku huu, Baba. Nakusihi kwa ajili ya watu hawa. Naombea kila mmoja wao, katika Jina la Yesu Kristo, Bwana. Naomba ya kwamba Kristo Mwana wa Mungu ataingia katika moyo wa kila mmoja wetu, Bwana, na kutufinyanga na kutufanya viumbe vipya katika Yesu Kristo. Tujalie, Bwana Mungu.

³³² Tunakupenda. Nasi tunataka maelekeo yetu . . . yetu . . . badiliko letu litujie sisi, tupate kuwa watoto Wako, tusikie Roho Wako akitenda kazi mioyoni mwetu, Bwana, akitufanya wepesi na kutufanya tung'amue nyakati hizi za wenda wazimu tunamoishi. Tujalie, Mungu. Tunapooni vijana wanawake wamenaswa katika wavu wa Ibilisi, vijana wanaume, nia zilizopotoshwa, watoto, waliolemewa na ulevi wa bangi, wavuta sigara, walevi, wenye utovu wa uadilifu, Edeni ya Shetani.

³³³ Mungu, ilikuchukua miaka elfu sita, kulingana na Biblia, kujenga Edeni. Nawe ukamweka mwanao na mkewe mle ndani (bibi-arusi wake) kuitawala. Naye Shetani akaja na kuipotisha; ana miaka elfu sita, naye amejenga Edeni yake ya kiakili kwa sayansi, na elimu, na inayodhamiwa kuwa akili, naye amejenga ikawa uchafu wa mauti.

³³⁴ Ee Mungu, turudishe Edeni tena, Bwana, ambako hakuna mauti, ambako hakuna huzuni. Tujalie, Bwana. Tunasimama kwa unyenyekevu, tusingoja Adamu wa pili aje kwa Bibi-arusi Wake. Tufanye sehemu Yake, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

³³⁵ Je, mnampenda Mungu? Je, mnaweza kusikia . . . Je, mnatambua ninayotaribu kuwaambieni? Kama mnaweza kufahamu hili hebu inueni mikono yenu tu, mkasema, "Ninafahamu yale unayotaribu kusema." Je, mnaweza kuona

wenda wazimu wa wakati huu? Tazama jinsi umesambaa, watu hawana akili tena. Imepotea! Wako wapi . . . ? Hata viongozi.

³³⁶ Tazama Rais wetu! “Iwapo wanataka Ukomunisti, hebu wapewe. Cho chote watu wanachotaka, na wapewe. Wako wapi akina Patrick Henry wetu, akina George Washington wetu? Wako wapi viongozi wetu wanaoweza kusimamia kanuni? Hatuna wao tena.

³³⁷ Wapi makanisa yetu, wahudumu wetu? Watawakubali watu tu kwa makatazo, au ingia . . . jiunge na kanisa na ufanye hivi, ama upate mwasho mdogo ama cho chote kile. Wako wapi hao watu wa Mungu, hao manabii wanaosimama kule na kuthubutu kuasi—kuasi mambo yote ya ulimwengu?

³³⁸ Wako wapi hao watu waaminifu? Wako mahali gani? Wamekuwa hafifu, na kupitia kwa mawazo ya akili na kadhalika, hata hawako hapa tena. Ee Mungu, uturehemu.

³³⁹ Vitu hivi vyenye sura ya kuogofya ambavyo vinakuja duniani. Mnaona jinsi watu wanavyoenda hata kwake. Ni wenda wazimu. Bali jambo hilo litakapotokea, Kanisa litakuwa limekwisha kuondoka.

³⁴⁰ Mungu, hebu tuwe huko. Hayo ndiyo maombi yangu kwa kile Kiumbe kikuu cha Kimbinguni kilicho humu jengoni usiku wa leo, yule Kristo mkuu ambaye yungali ana Uzima wa Milele. Nakuomba, Ewe Kristo, nikiwa humu huku nimefungua macho yangu, nikilitazama kanisa ambalo umeisha likombo kwa Damu Yako. Mungu usiache mmoja wetu akapotee. Tunataka kupatana nawe. Kwa hivyo utuoshe, Ee, Bwana, na maovu yetu yote. Ondoa dhambi zetu na kadhalika.

³⁴¹ Tumekuona Wewe ukiponya wagonjwa wetu, hata kuwafufua wafu wetu (wanafufuka kwa maombi), tumeona mambo haya yote yakitendeka, Baba. Sasa tufanye sisi tena tupate Uhai, kiroho; tufanye tena tupate kutambua Uzima wa Milele kupitia kwa Yesu Kristo. Tujalie haya, Baba. Nawakabidhi wote Kwako. Katika Jina la Yesu Kristo.

Hata tuonane huko juu,
Hata twonane Kwake Kwema;
Hata twonane huko juu, (Mtazame na hebu akufanye mwororo.)
Mungu awe nanyi daima.

³⁴² Tuinue mikono yetu sasa:

Hata twonane huko juu,



UONGOZI SWA65-1207
(Leadership)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne jioni, Desemba 7, 1965, kule Covina, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org